SportPesa
TZS. 517,350,800
CHEZA USHINDE JACKPOT
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



**KESI YA MBOWE**
Mshtakiwa adai kuteswa kuumizwa na askari polisi
UKURASA 3



UKURASA 11

Nipashe
Jumamosi Septemba 25, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580714
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Bosi TRA adai Sabaya hakutumwa kudai kodi

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan, akisaini kitabu cha kumbukumbu katika Ofisi za Umoja wa Mataifa jijini New York, Marekani, baada ya kuhutubia mkutano wa 76 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa juzi. Kushoto ni Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres. **PICHA: IKULU**

UKURASA WA 4

## WANYONGWA HADI KUFA KWA KUMUUA NA KUMFUKIA MTOTO

WATU wawili wakazi wa Kijiji cha Gwanumpu, Kakonko mkoani Kigoma, wamehukumiwa kunyongwa hadi kufa baada ya kukutwa na hatia ya mauaji ya mtoto wa miaka 12 waliyemteka wakidai wapewe Sh. milioni tano na baadaye kuuzika mwili wake ukiwa umekalishwa na...

UKURASA WA 4

## WAZIRI APIGA MARUFUKU UJENZI HOLELA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ameitaka Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, mkoani Dodoma, kuchukua hatua kuhakikisha maeneo hayo yanapangwa na...

# Masharti matano Rugemalira kudai fidia mahakamani haya

UKURASA 3

## Kishindo cha Samia UN, wadau wapongeza

UKURASA 2

MICHEZO WATANI WA JADI KUMALIZA UBISHI UK.24 | MAONI, KATUNI UK.6




Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makala, akizungumza wakati akifungua mkutano wa wamiliki wa viwanda, ulioandaliwa na Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania (CTI), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Bosi TRA adai Sabaya hakutumwa kudai kodi

**Na Allan Isack,** ARUSHA

KAIMU Meneja wa Mamlaka ya Mapato (TRA), Mkoa wa Arusha, Kayobio Majogoro (41), amedai katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha kuwa ofisi yake haikuwa na taarifa za aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, kuongoza kikosi maalum kwenda kufanya operesheni ya kukusanya kodi jijini Arusha.

Ofisa huyo wa mamlaka hiyo alitoa madai hayo mbele ya Hakimu wa mahakama hiyo, Patricia Kisinda, alipopanda kizimbani jana kutoa ushahidi katika kesi ya uhujumu uchumi namba 27 inayomkabili Ole Sabaya na wenzake sita.

Washtakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka matano ya matumizi mabaya ya madaraka, utakatishaji wa fedha, kujihusisha na vitendo vya rushwa, kuongoza genge la uhalifu na kujihusisha na vitendo vya rushwa.

Mbali na Sabaya, washtakiwa wengine katika shauri hilo ni Silvester Nyengu (26), Enock Togolani (41), Watson Mwahomange (27), John Odemba, Jackson Macha (29) na Nathan Msuya (31).

Akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Ofmed Mtenga, alidai mahakamani huko kwamba kwa mujibu wa sheria, Kamishna wa TRA ndiye mwenye mamlaka ya kuunda kikosi kazi maalum kwa ajili ya kukusanya na kuchunguza masuala ya kikodi.

Alidai suala la kukusanya kodi lipo chini ya mamlaka hiyo na vyombo vingine vya serikali na wananchi wanabaki kuwa ni wadau tu.

Shahidi huyo alidai vyombo vingine vya serikali vikiwamo vya dola vinashirikiana nao kwa kuwaomba kuwapatia msaada wa askari kama wanakwenda kufanya oparesheni maalumu za kukusanya kodi au kufanya uchunguzi.

Alidai kuwa kikosi kazi kikiundwa na Kamishina wa TRA, lazima mameneja wa mikoa wa mamlaka hiyo watajulishwa kwa kupewa taarifa juu ya ujio wa kikosi hicho.

Vilevile, alidai kwamba amekuwa Kaimu Meneja wa mamlaka hiyo mkoani humo tangu Mei, mwaka huu na kwa mujibu wa kitabu cha kuhifadhi kumbukumbu, hakuna kikosi maalum kilichotumwa Arusha kufanya operesheni ya kukusanya kodi.

"Kikosi kilichofanya kazi mwaka huu Arusha, ninakumbuka ni kikosi kimoja tu tena kilikuwa cha ndani cha maofisa wetu kilichoundwa na kamishina mwenyewe," alidai.

Alidai kuwa katika kukusanya kodi kwa mujibu wa sheria, mkuu wa wilaya hahusiki kabisa.

"Ikitokea mkuu wa wilaya amemkuta mfanyabiashara ambaye hatumii au hana mashine za kielekroniki (EFD), kazi yake ni kutupa sisi taarifa ili maofisa wa TRA tuchukue hatua za kisheria kwa kuwa ndio wahusika wakuu," alidai.

Kaimu meneja huyo alidai haifahamu operesheni ya Januari 22, mwaka huu inayodaiwa kufanya na Sabaya jijini Arusha ya kukusanya kodi kwa kuwa ofisi yake haina taarifa.

"Kikosi kazi maalumu hakiwezi kuundwa kwa ajili ya kufuatilia muamala mmoja kwa kuwa kuna mambo mengi ya kufanya ya kodi nchini, kikosi hicho kinaundwa pale inapohitajika," alidai shahidi huyo.

Alidai kuwa mbali na kuwa Kaimu Meneja wa TRA Mkoa wa Arusha, amekuwa ofisa wa ukusanyaji wa kodi kwa zaidi ya miaka 10.

Akihojiwa na Wakili wa Upande wa Utetezi, Mosses Mahuna, shahidi huyo alidai anafahamu maana ya vishoka au matapeli wa kodi kuwa ni watu ambao wanahusika kuwasaidia wateja bila ya kuwa na usajili wa TRA kwa mujibu wa sheria.

# Kishindo cha Rais Samia UN, wasomi na wadau wampongeza

**Na Waandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, juzi alihutubia Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UNGA) na kubainisha mikakati ya Tanzania kushirikiana na mataifa mengine kutatua matatizo yanayoikabili dunia ikiwamo UVIKO-19.

Rais Samia ambaye alianza kuhutubia saa 2:42 usiku, alilieleza baraza hilo kuwa ugonjwa UVIKO-19 bado unaendelea kupunguza kasi ya kufanikisha Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) katika muda uliopangwa na kwamba katika baadhi ya nyanja, taarifa zinaonyesha kuwa kumekuwa na athari zilizorudisha nyuma mafanikio yaliyopatikana.

Alitoa mfano kuwa takriban watu milioni 71 duniani wanatarajiwa kurejea kwenye umasikini licha ya kwamba walishaondokana na hali hiyo.

Alibainisha kuwa tangu kuanza kwa UVIKO-19, Tanzania imekuwa ikichukua jitihada mbalimbali kukabiliana nao na Julai mwaka huu, alizindua rasmi mpango ya chanjo nchi nzima.

Rais Samia alisema ili watu wengi katika nchi zinazoendelea waweze kupata chanjo, ni vyema hakimiliki ya kuzalisha chanjo hizo itolewa ili uzalishaji ufanyike kwenye nchi nyingi.

Rais Samia pia alitumia hotuba hiyo kueleza juhudi za serikali katika kukuza uchumi, licha ya vikwazo vya ugonjwa huo na kwamba baada ya kushuka kwa ukuaji uchumi kutoka asilimia 6.9 hadi asilimia 5.4, hivi sasa Tanzania inafanya jitihada za kuziinua sekta zilizoathirika zaidi na ugonjwa huo ikiwamo ya utalii.

Alisema pia serikali inaimarisha mazingira ya kufanya biashara ili kuvutia uwekezaji nchini pamoja na kuimarisha misingi ya utawala bora.

Rais Samia pia aliweka wazi mikakati ya serikali katika kuongeza ushiriki wa wanawake katika nyanja za uchumi ikiwa ni pamoja na kuweka sera madhubuti na maboresho ya mfumo wa bajeti ili kupunguza idadi ya wanawake na wasichana wanaoishi katika umaskini.

Kuhusu athari za mabadiliko ya tabianchi, Rais Samia alisema kuna umuhimu wa kuchukua hatua za kukabiliana na janga hilo na kuyasisitiza mataifa yaliyoendelea kutimiza ahadi zao za kutoa Dola za Marekani bilioni 100 kwa mwaka ifikapo mwaka 2025 kama ilivyokubaliwa katika Azimio la Paris.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Shule ya Sheria, Ebeneza Mshana, alisema wamefarijika na wanatembea kifua mbele baada ya Rais Samia kuhutubia UN.

Mkurugenzi wa asasi isiyo ya kiserikali ya Tree of Hope kutoka Tanga, Fortunata Manyenesa, alisema wamefarijika kuona kwa mara ya kwanza Rais wa Tanzania mwanamke anahutubia katika baraza hilo.

Pia alisema mada alizobeba za mabadiliko ya tabianchi na corona ni matatizo ya kidunia ambayo yamemfanya kuonyesha umahiri na utayari wa kuungana na jumuiya za kimataifa katika kukabiliana na matatizo hayo.

Mkurugenzi wa kwanza mstaafu wa Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika (WiLDAF), Dk. Judith Odunga, alisema Rais Samia ameibeba nchi kimataifa na kwao watetezi wa haki za wanawake, wanaona amefanya vizuri.

**■Imeandaliwa na Mary Geofrey na Romana Mallya**

## Ummy: ma-DED chanzo wanawake kupigana ofisini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, amedai kuwa amebaini kuwapo wakurugenzi wanaume kutumia vyeo kujihusisha kimapenzi na watumishi wa kike.

Amesema tabia ya wakurugenzi hao inasababisha baadhi ya watumioshi kupigana kwa sababu yao.

Aidha, amewapa tumbo joto wakurugenzi wapya 61 wa halmashauri walioteuliwa, hivi karibuni na Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwaambia kuwa wako chini ya uangalizi kwa miezi sita wakipimwa utendaji kazi wao.

Waziri Ummy aliyasema hayo jana kwenye mafunzo elekezi kwa wakurugenzi wa mamlaka za serikali za mitaa nchini na kusisitiza, kuwa hatavumilia uonevu na udhalilishaji, dhidi ya wanawake kwa kisingizio cha cheo cha ukurugenzi.

"Mimi Waziri ninayemsaidia Rais sitavumilia suala hilo. Sasa umekuwa mkurugenzi kila mfanyakazi mzuri kwenye halmashauri yako ni wako. hii hapana.

"Hili ni moja ya mada Katibu Mkuu atalisema hapa. Hatuwezi kwenda hivyo hawa ni binadamu lakini tunazo kesi wakurugenzi wanasababisha watumishi wanawake wanapigana kisa mkurugenzi. Mtu wa aina hii hafai wala hatoshi kuwa mkurugenzi," alisema huku akisema bado hajapata kesi za wakurugenzi wanawake.

"Sijapata kesi za wanawake, lakini wanawake wenzangu twende tukajiheshimu. Hii ni nafasi kubwa sana, siyo leo upo na huyu, kesho na huyu haileti taswira nzuri kwa kiongozi wa umma katika nafasi," alisema huku akiwataka wakurugenzi wanawake kulinda utu na heshima waliyopewa na rais na kuangalia watu wanaotoka nao kimapenzi.

"Kuna mwingine ametongozwa amekataa basi hapelekwi semina. Anahamishwa kisa amemkataa mkurugenzi. Hebu tafuta nje ya halmashauri, lakini isiwe chanzo cha wanawake kupigana maana posho nayo huwa kubwa unajengewa nyumba, wanapewa gari inabidi wanawake tu wapigane,"alisema.

Kuhusu wakurugenzi wapya, Waziri Ummy alisema wako chini ya uangalizi kwa miezi sita na wanapaswa kuonyesha uwezo wao, kwenye utendaji kazi kwa kuwa waliteuliwa kwa kuangalia wasifu na utendaji kazi wao, maeneo waliyokuwapo awali.

"Niseme bila kupepesa macho, mpo kwenye uangalizi na tutapima utendaji wenu kwa sababu mliteuliwa kwa kuangalia, CV (wasifu) na utendaji wa huko mlikokuwa. Sasa kwenye kazi ya ukurugenzi ni watu ambao mtamsaidia Rais Samia kusimamia shughuli za utawala na maendeleo kwenye mamlaka za serikali za mitaa. Hatuwatishi mpo kwenye uangalizi baada ya miezi sita mimi na Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu tutapeleka taarifa kwa rais, atafanya uamuzi," alisema.

## HABARI KITAIFA

### KESI YA MBOWE

# Mshtakiwa adai kuteswa, kuumizwa kituoni polisi

**Na Kulwa Mzee**

MSHTAKIWA wa pili katika kesi ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe na wenzake watatu, Adamu Kasekwa, amedai Polisi walimwekea dawa za kulevya na bastola baada ya kumkamata.

Kasekwa pia amedai Sh. 260,000 alizokuwanazo mfukoni wakati anakamatwa, zilichukuliwa na Kamishna Msaidizi wa Polisi Ramadhani Kingai na hajaandikiwa risiti ya fedha hizo.

Alibainisha hayo jana Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi mbele ya Jaji Mustapha Siyani wakati shahidi wa kwanza wa upande wa Utetezi alipoanza kujitetea katika kesi ndogo baada ya Jamhuri kufunga ushahidi wakiwa na mashahidi watatu badala ya saba waliowataja awali.

Akiongozwa na Wakili John Mallya, Kasekwa alidai alifahamiana na mshtakiwa Mbowe wakati anahitajika kwa ajili ya kazi ya ulinzi mwishoni mwa Julai 2020.

Alidai walikuwa wako katika mazungumzo ya kujaza mkataba wa kazi ikijumuisha malipo na majukumu watakayokuwa nayo, walikutana Moshi.

Kasekwa alidai kuwa Agosti 5 mwaka jana, akiwa na mshtakiwa wa tatu, Mohammed Ling'wenya, maeneo ya Lau Madukani, walivamiwa na watu zaidi ya watano.

Alidai walianza kumpiga, wakachukua silaha waliyokuwa nayo na dawa za kulevya wakamwekea kisha akawasikia wanasema wamemkuta na vitu hivyo, maneno ambayo mshtakiwa mwenzake Ling'wenya aliyasikia.

"Ling'wenya alitoa vitu vyake mfukoni huku akisema mwenzangu mmeshamwekea dawa na silaha, mimi ninatoa vitu vyangu kabisa.

"Walionishambulia niliwaona wawili hapa mahakamani, ACP Ramadhani Kingai na Inspekta Mahita Omary, niliwafahamu kwa sura, majina nimeyafahamu humu mahakamani," alidai Kasekwa.

Alidai kuwa wakati akiongea na simu, mara askari wakamvamia kumkamata, askari mmoja alikuwa na kitu akaingiza katika mfuko wake wa suruali na kutoa akasema alimkuta na dawa na mwingine alikuwa na silaha akaibana katika mkanda wake wa suruali akatoa na kudai alimkuta nayo.

Shahidi anadai alipigwa, walifungwa pingu wote na kuingizwa katika gari kupelekwa Kituo cha Polisi Moshi.

"Polisi Moshi walinichukua wakanipeleka katika nyumba ya pembeni, walinivua nguo zote, walichukua bomba wakanining'iniza kama popo, walinipiga huku wakiuliza nilifuata nini Moshi, niliwajibu nilifata kazi ya ulinzi kwa Mbowe, majibu yangu hayakuwaingia kichwani, waliendelea kunipiga na kuuliza swali hilo hilo," alidai.

Kasekwa alidai ilichukua dakika 30 ama 45 kupitia mateso hayo na alikuwa hawezi kusimama, hivyo walimvalisha suruali, shati walimwekea begani, wakamkokota hadi mahabusu, wakamfunga pingu miguuni na mikononi wakamfungia humo na ilipofika jioni aliingia askari akamwaga maji.

Shahidi alidai kuwa siku iliyofuata, alitolewa mahabusu na akabaini ilikuwa mchana alipoona jua, alifungwa jaketi usoni akapakiwa kwenye gari na hakujua alikokuwa anapelekwa.

Alidai kuwa akiwa kwenye gari, alikuwa anachomwachomwa kwa bisibisi huku akiambiwa anakoelekea ndio mwisho wa maisha yake.

Alidai alikaa chini katika safari hiyo na alikuwa anaungua kwa kuwa gari lilikuwa linatoa moto pale chini, na walipofika alikokuwa anapelekwa, alivuliwa jaketi.

Kasekwa alidai aliachwa ndani kwa muda mrefu akiwa na pingu, akajikokota hadi mlangoni akaona mahabusu wengine wengi, akawauliza wako wapi, wakamwambia Kituo cha Polisi Tazara na kituo hicho kinakaa watuhumiwa wa ugaidi. Alidai alikaa Tazara tangu Agosti 7 hadi 9 usiku alipochukuliwa na kupelekwa Kituo cha Mbweni, akidai jina hilo la kituo alitajiwa na askari aliyemkuta huko.

Siku iliyofuata usiku, aliingia Kingai na Goodluck na aliambiwa na Kingai kwamba akiona mateso yanapungua mapumziko yanakaribia na kumtaka awe mstaarabu na anamfungua pingu ili kutia saini nyaraka walizokuwa nazo.

Alidai alichomwambia ndicho akichokuwa anatekeleza na alipotakiwa kuonyesha sehemu alizoumizwa, alionesha makovu kwenye mguu wa kushoto na mkono wa kushoto. Akihojiwa na Wakili wa Utetezi, Nashon Nkungu, Kasekwa alidai fedha zake alichukua Kingai na hajapewa risiti na bisibisi alichomwa katika mbavu na kwenye makalio.

Wakili Peter Kibatala alihoji kama wakati anakamatwa Kingai alikuwapo, shahidi akidai alikuwapo na ndiye aliyechukua fedha zake.

Shahidi alionyesha suruali aliyovaa jana mahakamani akidai ndiyo aliyokuwa amevaa wakati anakamatwa, ikiwa imekatika vishikizo isipokuwa kimoja na kaifunga kamba.

Alidai hakuna shahidi aliyefika mahakamani kuzungumzia fedha zake na aliongeza kuwa katika mahabusu ya Tazara aliwakuta watu wawili ambao anawafahamu kwa haiba, mmoja alikuwa Msomali aliyevaa kanzu na mwingine mwanajeshi wa Jeshi la Wananchi Tanzania Kikosi cha Twalipo, waliokuwa wanashikiliwa kwa tuhuma za ugaidi. Shahidi alidai kuwa Agosti 19, mwaka jana alikutana na Ling'wenya na Halfani Bwire katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu. Hakuwahi kukutana na Ling'wenya mahali pengine tangu walipokamatwa Moshi Agosti 5, mwaka jana.

Upande wa utetezi unatarajia kuwa na mashahidi wanne, akiwamo mshtakiwa wa pili katika kesi ndogo ambapo upande huo unapinga maelezo ya onyo yasipokewe kwa madai kabla na wakati maelezo yanachukuliwa, mshtakiwa Kasekwa aliteswa.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Mbowe, Adamu, Mohammed na Bwire ambao wanashtakiwa kwa mashtaka sita yakiwamo ya kula njama, kulipua vituo mbalimbali vya mafuta na kuwadhuru viongozi wa serikali.

# Masharti matano Rugemalira kudai fidia mahakamani

**Na Kulwa Mzee**

KUACHIWA huru kwa mfanyabiashara James Rugemarila baada ya kukaa gerezani bila kesi kuanza kusikilizwa kwa zaidi ya miaka minne kumezua mjadala huku mawakili wakisema katika mazingira hayo, anaweza kudai fidia kwa madhara aliyopata.

Hata hivyo, wataalamu hao wa sheria wana angalizo kwamba itakuwa ngumu kwa mfanyabiashara huyo kushinda kesi hiyo ya madai ya fidia, wakilinganisha na dhana ya 'ngamia kupenya kwenye tundu la sindano'.

Katika mazungumzo na Nipashe kwa nyakati tofauti mkoani Dar es Salaam, mawakili wa kujitegemea walisema mhusika baada ya kuachiwa huru, anaweza kudai fidia, lakini tayari Mahakama ya Rufani ilishatoa vigezo vitano kwa kuzingatiwa na endapo mhusika atakidhi, anaweza kudai fidia mahakamani.

Wakili Benedict Ishabakaki aliiambia Nipashe kuwa mtu aliyekamatwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma, akafunguliwa mashtaka mahakamani na baada ya kukaa mahabusu kwa muda mrefu kesi inafutwa kwa kukosekana kwa ushahidi anaweza kudai fidia.

"Ukiachiwa na ukawa umepata madhara yoyote, unafungua kesi dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kudai fidia," alisema.

Wakili huyo alirejea uamuzi wa Mahakama ya Rufani katika kesi ya Jeremiah Kamama dhidi ya Bugomola Mayandi, rufani namba 4 ya mwaka 1981, vilipotolewa vigezo vya kudai fidia.

"Ili udai fidia kuna vigezo vitano: Cha kwanza kesi husika lazima iwe imesikilizwa; pili, mhusika awe ameshinda kesi; tatu, mhusika afungue madai ya fidia; nne, kama hakukuwa na sababu inayofaa na inayowezekana kuwapo kwa mashtaka kama hayo; na kigezo cha tano mhusika lazima aoneshe madhara aliyopata, mfano kwa kukaa mahabusu muda mrefu alikosa kazi au madhara mengine aliyopata," alifafanua.

Alipoulizwa kuhusu suala la Rugemarila kama anaweza kukidhi vigezo au la, Wakili huyo alisema mfanyabiashara huyo alifutiwa mashtaka, hivyo ni ngumu kwa vigezo hivyo kushinda kesi ya kudai fidia, lakini anaweza kufungua shauri akadai fidia.

Wakili Majura Magafu akizungumzia suala hilo, alisema DPP anapofuta kesi na kumwachia huru mhusika, aliyeachiwa anayo haki ya kupeleka madai mahakamani ili alipwe fidia kwa madhara aliyoyapata kwa muda wote huo aliokaa mahabusu.

"Mahakama itakapojiridhisha na madai inaweza kuamua alipwe," alisema Wakili Magafu.

Wakili Casto Rweikiza, akifafanua zaidi kuhusu suala hilo, alisema mtuhumiwa anapopelekwa mahakamani mbele ya hakimu na kusomewa mashtaka, upelelezi unatakiwa kufanyika ndani ya siku 60.

Alisema siku hizo zikiisha, mahakama yenyewe kwa kuliona ama kwa washtakiwa kupitia mawakili wao kuwasilisha maombi, mahakama inaweza kuliondoa shauri hilo.

"Endapo itatokea wanahitaji kuongeza muda, Mkuu wa Upelelezi kupitia Mawakili wa Serikali, anawasilisha maombi ya kuongeza muda wa upelelezi, maombi hayo anatakiwa kuwasilisha akiwa ndani ya siku 60," alisema Wakili Rweikiza.

Alisema kwa kukaa mahabusu gerezani miaka mingi bila kesi kuendelea kisha DPP anamwachia huru mtuhumiwa, mhusika anaweza kudai fidia.


## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Access Microfinance Bank Tanzania Limited kupitia Kampuni za Madalali itauza kwa njia ya mnada wa hadhara, Nyumba, Viwanja na Magari vilivyowekwa kama dhamana ya mikopo ambapo wateja husika wameshindwa kulipa mikopo yao kwa mujibu wa mikataba husika. Hivyo basi ifahamike kuwa utakapopita muda wa siku kumi na nne (14) tangu kutoka kwa tangazo hili, dhamana husika zitauzwa kwa njia ya mnada. Mnada utafanyika sehemu nyumba na viwanja husika vilipo siku na tarehe kama vilivyotajwa kwenye jedwali hapo chini.

| NA. | JINA LA MTEJA | TAWI HUSIKA | JINA LA MWENYE DHAMANA | AINA YA DHAMANA | ENEO DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | SAID/HAMOUD, SAID | KAHAMA | MKOLE/CHRISTOPHER ROSEMARY | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO (ALTERNATIVE MORTGAGE) & HOME ASSETS | KAHAMA | **16/10/2021 SAA 4:00 ASUBUHI** |
| 2 | KAPELA/SHABANI ,RAMADHANI | TABORA | KAPELA/SHABANI, RAMADHANI | HATI NAMBA 246 TBRLR | TABORA -ISEVYA | **16/10/2021 SAA 4:00 ASUBUHI** |
| 3 | MWAMAKULA/ A,GEOFREY | PAMBA | MWAMAKULA/A, GEOFREY | HATI NAMBA 31773 NA GARI NAMBA T 959 CBM | ILEMELA-KISEKE | **16/10/2021 SAA 4:00 ASUBUHI** |
| 4 | MSUFU/DAUDI, MICHAEL | TABORA | MSUFU/DAUDI, MICHAEL | GARI YENYE NAMBA T 896AMR | TABORA | **16/10/2021** |

1. UKAGUZI UNARUHUSIWA MARA USOMAPO TANGAZO HILI.
2. MNUNUZI ATALAZIMIKA KULIPA MALIPO YA 25% YA FEDHA TASLIMU PAPO HAPO NA 75% BAADA YA SIKU 14 TOKA SIKU YA MNADA KUFANYIKA NA KUSHINDWA KULIPA MALIPO YALIYOBAKI MNADA UTARUDIWA NA FEDHA ULIZO LIPA HAZITARUDISHWA
3. GHARAMA ZA KUBADILISHA UMILIKI NI ZA MNUNUZI MWENYEWE, KUMBUKA VIGEZO NA MASHARTI KUZINGATIWA.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI**
**ACCESS MICROFINANCE BANK TANZANIA LIMITED SIMU NAMBA. +255 677 860 000**
**WOTE MNAKARIBISHWA.**

216477002

# Wanyongwa hadi kufa kwa kumuua na kumfukia mtoto

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

WATU wawili wakazi wa Kijiji cha Gwanumpu, Kakonko mkoani Kigoma, wamehukumiwa kunyongwa hadi kufa baada ya kukutwa na hatia ya mauaji ya mtoto wa miaka 12 waliyemteka wakidai wapewe Sh. milioni tano na baadaye kuuzika mwili wake ukiwa umekalishwa na kufungwa kichwani, usoni na miguuni.

Waliohukumiwa kwenye kesi hiyo ya mauaji ya kukusudia namba 18/2021 katika Mahakama Kuu kanda ya kigoma ni Tabibu Nyundo na Thobias Mtakiyicha. Walidaiwa kutenda kosa hilo Januari 27, 2019 baada ya kumteka mtoto na kutuma ujumbe mbalimbali wa simu kwa jirani wa wazazi wa mtoto.

Sehemu ya ujumbe ulisomeka" "Tumemkamata mtoto wa Buchumi tunataka Sh. milioni tano mwambie baba yake atume pesa hizo ili tumwachie."

Upande wa Jamhuri ukiongozwa na mawakili Happiness Mayunga na Antia Julius, uliwakilishwa na mashahidi tisa wakiwamo baba mzazi, jirani aliyetumiwa ujumbe wa simu, ofisa mtendaji, mwenyekiti wa kijiji, askari polisi na daktari.

Ilielezwa wakiwa kwenye harakati za kumtafuta mtoto bila mafanikio, Januari 30, 2019 walilazimika kuchangisha fedha kwa wanakijiji na kupatikana Sh. 700,000 na mzazi wa mtoto kuongezea Sh. 800, 000 hivyo kufikia Sh. Milioni 1.5 ambazo walizituma kwa namba iliyotuma ujumbe huo baada ya kukubaliana kushusha kiwango kutoka Sh. milioni tano.

Ilipofika Februari 2, 2019 walikwenda ofisi za watoa huduma wa simu kuifuatilia namba waliyoitumia pesa na kubainika fedha hizo zilitumwa kwenda kwa Thobias Mtakiyicha ambaye wanamfahamu na kuanza jitihada za kumtafuta nyumbani kwake.

Walidai kuwa baada ya kufika kwake hawakumkuta na kupewa maelekezo alikokwenda yeye na rafiki yake shambani, hivyo kuchukua hatua za kumfuatilia lakini walimpata rafiki yake na alionekana mwenye wasiwasi na alipo ulizwa juu ya mwenzake, alisema yuko njiani akirejea nyumbani na laini ile iliyotumiwa fedha anayo.

Hatua hiyo, walidai kuwa ilisaidia kupatikana fedha hizo ambazo zilitolewa kwenye simu kisha kutumika kama kielelezo cha shauri hilo. Wakiwa rumande Februari 6, mwaka huo, shahidi wa tisa wa Jamhuri alidai kuwa aliitwa na mmoja wa washtakiwa hao na aliposogea walimwambia tunaomba waseme ukweli ndipo wakaweka wazi kuwa walimteka mtoto kisha kumwua na kumzika na kwamba wako tayari kwenda kuonyesha eneo hilo.

Ilidaiwa kuwa polisi waliwachukua hadi eneo alipozikwa mtoto kisha kuwarudisha washtakiwa na baadaye kwenda na wanakijiji pamoja na familia ya mtoto kufukua kaburi hilo ambalo walikuta mwili ukiwa umezikwa.

Washtakiwa wakitetewa na mawakili wawili Sylvester Sogomba na Elizabeth Twakazi, walikana mashtaka hayo na kudai ni ya uongo na utetezi wao kwa uchache walidai wameunganishwa kwenye kesi wakati hawafahamiani.

Pia walidai maelezo yaliyowasilishwa na polisi si ya kweli waliyatoa baada ya mateso makali waliyopewa na kuwa mmoja ya mshtakiwa alikuwa na mgogoro na baba wa mtoto, hivyo kuna uwezekano ametumia mwanya huo kumsingizia.

Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Kigoma, Lameck Mlacha, aliyekuwa akisikiliza kesi hiyo, alisema washtakiwa wamedanganya mahakama kuwa hawafahamiani wakati ni vijana wanaoishi kijiji kimoja.

Kuhusu madai kuwa walipigwa na polisi pasipo kutoa vielelezo vyovyote vya kiafya pia maelezo waliyompatia askari polisi yalijawa hatia na kujuta na yalifanikisha kupatikana kwa mwili wa mtoto pamoja na laini ya simu iliyotumiwa fedha kukutwa nayo.

"Adhabu ni moja tu kunyongwa hadi kufa. Hii adhabu siipendi lakini mikono yangu imefungwa. Nafasi ya rufani iko wazi," alisema Jaji Mlacha.

## Wanne familia moja wafariki kwa radi

**Na Lilian Lugakingira,** MULEBA

WATU wanne wa familia moja wamepoteza maisha kwa kupigwa na radi, kutokana na mvua iliyonyesha usiku wa kuamkia juzi, katika kisiwa cha Bumbile kilichoko Ziwa Victoria upande wa Wilaya ya Muleba, mkoani Kagera.

Mkuu wa Wilaya ya Muleba, Thoba Nguvilla, alisema mvua hiyo ilinyesha wakati watu hao, ambao ni baba mwenye nyumba, mke na watoto wao wawili wa kike wakiwa bado wamelala.

Nguvilla aliwataja waliopoteza maisha kuwa ni Sylvester Richard na mke wake Veronica Richard pamoja na watoto wao wawili, ambao majina yao hayakupatikana mara moja. Wote ni wenyeji wa Kisiwa cha Ukerewe, mkoani Mwanza.

"Miili ya wanafamilia hao, ambao walitoka Ukerewe kuja kufanya shughuli za kilimo na uvuvi katika kisiwa cha Bumbile, tayari imesafirishwa kwenda Ukerewe, kwa ajili ya mazishi," alisema Nguvila.

Kutokana na tukio hilo, Nguvilla aliwaomba wananchi katika kisiwa hicho na wilaya nzima kwa ujumla kuchukua tahadhari kwa kukaa sehemu salama pindi mvua zinapoanza kunyesha, ili kupunguza madhara yanayoweza kutokea kutokana na mvua ikiwamo kupigwa na radi.

Mwenyekiti wa kitongoji cha Bulyo lilikotokea tukio hilo, Robert Musiibha, alisema nyumba walimokuwa wamelala watu hao, ambayo ilikuwa imejengwa kwa mabanzi na kuezekwa kwa mabati, nayo iliteketea kutokana na moto wa radi hiyo.

"Wananchi walijitahidi kutoa msaada, lakini kutokana na ukubwa wa moto walishindwa kwa kuwa tukio lilitokea watu wakiwa bado wamelala. Labda kama ingekuwa mchana wangeweza kuokolewa," alisema. Musiibha alisema radi hiyo ilipiga kwa nguvu na kuwashutua, lakini kwa kuwa wamezoea maeneo yao kupigwa na radi za namna hiyo, hawakufahamu haraka kama imesababisha madhara makubwa ya namna hiyo. Alisema watoto waliopoteza maisha wanakadiriwa kuwa na umri kati ya miaka mitano na sita.

Alisema tukio hilo ni la pili na kwamba la kwanza lilipiga katika Shule ya Msingi Kitua, lakini halikusababisha kifo na kwamba baada ya tukio hilo, aliiomba serikali kuangalia uwezekano wa kuweka mitego ya radi katika kisiwa hicho, ili kunusuru maisha ya wananchi.

"Katika msimu wa mvua watu huku wanaishi kwa hofu, kwa sababu radi ni nyingi mno na zinatisha. Sasa zimechukua maisha ya wenzetu, ambao tumeishi nao huku karibia miaka 10. Naomba serikali itusaidie kupata mitego ya radi, ili tuishi kwa amani," alisema mwenyekiti.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, akifungua kongamano la wadau kuhusu ukatili na udhalilishaji dhidi ya wanawake katika maeneo ya kazi, lililoandaliwa na Shirika la Wanawake Katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika (WiLDAF), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Naibu Waziri apiga marufuku ujenzi holela

**Na Munir Shemweta,** CHAMWINO

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ameitaka, Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, mkoani Dodoma, kuchukua hatua kuhakikisha maeneo hayo yanapangwa na kupimwa, ili kuepuka ujenzi holela.

Amesema eneo la Chamwino liko Ikulu, linahitaji kuwa na mpangilio mzuri utakaoainisha matumizi ya kila eneo na kusisitiza, kuwa halmashauri lazima ianze mikakati ya kuandaa mpango kabambe wa mji.

Dk. Mabula alisema hayo jana kwa nyakati tofauti wakati akizungumza na watendaji wa sekta ya ardhi na wananchi wa Kijiji cha Chamwino Ikulu, akiwa katika mwendelezo wa ziara yake katika Wilaya za Mkoa wa Dodoma.

Kwa mujibu wa Dk. Mabula, ujenzi unaofanyika Chamwino ni lazima uendelezwe kwa kuzingatia mipango miji na si wananchi kujenga holela wakati ni eneo la sura ya Ikulu, hivyo kuitaka halmashauri kuhakikisha maeneo yote yanapangwa, kupimwa na kumilikishwa.

Aidha, aliitaka Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino kuwatumia wenyeviti na watendaji wa kata, kusimamia ujenzi kwenye maeneo na kusisitiza kuwa mwananchi yeyote anayefanya ujenzi ni lazima aulizwe kibali na ramani, ili kudhibiti ujenzi holela.

"Chamwino haiwezi kukaa bila 'master plan' (mpango kabambe) wakati Ikulu ipo na sura ya nchi ni mahali ilipo Ikulu," alisema Dk. Mabula.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri, eneo la Ikulu kuzungukwa na maeneo yasiyopangwa Wizara ya Ardhi itakuwa haitendei haki Ikulu na kufafanua kuwa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), limeonyesha mfano kwa kuteleleza ujenzi wa ghorofa nane, zenye nyumba 100.

Naibu Waziri Mabula, ambaye aligawa jumla ya hati 298 kwa wamiliki wa ardhi waliorasimishiwa makazi holela kwenye kijiji cha Chamwino, aliwataka wananchi wa eneo hilo kuelewa kuwa wako kwenye uso wa Ikulu, hivyo hawawezi kuachwa kuendelea na ujenzi holela.

Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Dodoma, Thadei Kabonge, alisema Chamwino ni moja ya halmashauri zenye bahati nchini kwa kuwa na watumishi wa kutosha, pamoja na vitendea kazi vya sekta ya ardhi likiwamo gari.

Aliitaka halmashauri hiyo, kutumia fursa waliyo nayo katika kuongeza kasi ya umilikishaji ardhi na kuongeza kuwa halmashauri lazima inahakikisha kila mwenye ardhi anamilikishwa kwa lengo la kuongeza mapato ya sekta ya ardhi.

Naye Mkuu wa Idara ya Ardhi katika Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, Enock Mligo, alisema katika kutekeleza matumizi bora ya ardhi, kwenye halmashauri hiyo, tayari vijiji 13, vimefanyiwa mpango, ili kuepuka migogoro. Aliongeza kuwa ofisi yake imekuwa ikitoa elimu ya uandalizi wa mipango ya awali inayoainisha maeneo ya wakulima, wafugaji pamoja na yale maeneo ya hifadhi.

## TANGAZO
















# Dickson ashinda Gawio KUBWA kutoka betPawa la Toyota RAV4

betPawa wamekamilisha ndoto ya mteja wao na pia wamemtambulisha Mr Eazi kama balozi wao mpya.

Dickson alishinda pambano la upigaji wa penati lililofanyika katika hoteli ya Hyatt Regency Dar es Salaam na aliondoka na gari aina ya Toyota RAV 4 mpya kabisa. Alipata fursa ya kupatiwa zawadi ya funguo la gari hilo na Mr Eazi katika hafla iliyofana.

Mkazi huyo wa Shinyanga aliwashinda wenzake Jackson, Sadam, Nasibu, Titus, Robert, Bakari na Peter. Watano katika yao walijinyakulia Playstation 5 na wawili walijipatia vocha za manunuzi za supamaketi ya Shoppers zenye thamani ya TSH500,000 kila mmoja.

Washindi wote nane waliingia katika droo ya upigaji wa penati baada ya kuweka bashiri katika mechi ya Ligi kuu Uingereza mwezi Agosti.

Dickson alisema: ‘’Ninaishi katika moja ya ndoto zangu KUBWA. Nilikua nikiendesha magari used, lakini sahivi naendesha kitu kipya kabisa. Inanifanya nijisikie mtu wa tofauti kabisa’’.
‘’Nilipenda uwepo wa balozi aliyetambulishwa leo hapa Mr Eazi. Nimefurahi sana kumuona.’’

Fahamu zaidi kuhusu betPawa kwa kutembelea **betpawa.co.tz**

**betPawa**

Cheza kiasi. 18+. betPawa imesajiliwa chini ya bodi ya michezo ya kubashiri ya Tanzania. Leseni #SBI000000026

216476202

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Simba, Yanga wapeni raha mashabiki wenu

**MSIMU** mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara wa mwaka 2021/2022 unatarajiwa kuanza leo kwa mechi rasmi ya ufunguzi ya kuwania Ngao ya Jamii.

Mechi hiyo inayotarajiwa kuchezwa kuanzia saa 11:00 jioni kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam, itawahusisha watani wa jadi, Simba na Yanga.

Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), limetangaza waamuzi wa mechi hiyo watakuwa ni Ramadhani Kayoko atakayesaidiana na Frank Komba na Sudi Lila wakati mwamuzi wa akiba ni Elly Sasii, wote kutoka jijini.

Kwa mwaka huu, watani wa jadi watakuwa wanakutana kwa mara ya nne, tena michezo ikifanyika ndani ya muda mfupi. Mara ya mwisho timu hizo zilikutana Julai 25, mwaka huu kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani Kigoma.

Ilikuwa ni kwenye fainali ya Kombe la FA na Simba walifanikiwa kuibuka washindi. Bao pekee katika fainali hiyo lilifungwa na beki Mganda, Thadeo Lwanga.

Tunafahamu timu zote zimefanya maandalizi mbalimbali kuelekea mchezo huo, wakianzia kwenye kuboresha vikosi vyao kwa kusajili wachezaji wapya pamoja na kuimarisha mabenchi ya ufundi ili kusaka mafanikio bora zaidi.

Katika hili, Nipashe tunapenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza viongozi wa timu hizi mbili, pia na wa klabu nyingine zinazotarajia kushiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, Championiship (zamani Ligi Daraja la Kwanza), First League (zamani Ligi Daraja la Pili), kwa kufahamu mafanikio ya mpira yanatokana na uwekezaji.

Timu zilizofanya vyema katika eneo hili, hakika zinatarajia kuvuna matokeo chanya katika mashindano wanayoshiriki, lakini pia ikitekeleza vyema programu za mazoezi wakati wa kipindi cha 'pre season'.

Lakini yote haya yaweze kuonekana ni muda mwafaka kwa wachezaji kujituma na kucheza kwa kiwango cha juu na hatimaye kuisaidia timu kuvuna kile ambacho inakihitaji.

Kwa sababu ni mchezo ambao unahitaji kupata mshindi, kila mchezaji anatakiwa kujiandaa kupambana kuhakikisha wanatimiza malengo mazuri ya klabu yake lakini pia kutangaza vipaji vyao.

Mechi hii si tu inasubiriwa na wadau wa soka wa hapa nchini, lakini pia inafuatiliwa na makocha, mawakala na mashabiki wa mchezo huo wa sehemu mbalimbali duniani, hivyo wachezaji watakaopata nafasi wasiitumie vibaya kwa ajili ya kuweka mbele maslahi binafsi.

Wachezaji wakumbuke kama Luis Miquissone wa Simba ameweza kununuliwa kwa dau kubwa la fedha akitokea hapa nchini, badi ipo fursa ya nyota wengine kuuzwa, na ili yote haya yafanikiwe, kila mchezaji aweke akilini mwake kwamba kuna wakala amekuja kufuatilia kiwango chake.

Kwa kufanya hivyo, tunatarajia kuona kandanda la kiwango cha juu, nidhamu ya kiwango cha juu, burudani kama ambavyo mchezo wenyewe unavyojulikana lakini pia kuipa heshima TFF ambayo inasimamia soka hapa nchini.


Waamuzi ambao wamepewa dhamana ya kuuchezesha mchezo huu wanatakiwa kuhakikisha wanazisimamia vyema sheria 17 na kwa kufanya hivyo, kutaondoa malalamiko na kile kinachoitwa ushindi wa 'makandokando'.

Timu itakayofanya vyema ndio itatakiwa kubeba ngao hiyo na kuanza msimu mpya kwa kichezko.

Tunawakumbusha pia mashabiki kufahamu mipaka yao na kamwe wasigeuke makocha au kuwalaumu viongozi mara baada ya timu kupoteza mchezo.

Inafahamika wazi mchezo wa soka una matokeo matatu ambayo ni kufunga, sare au kupoteza mchezo. Pia wasisahau msemo maarufu wa mchezo wa soka una matokeo katili.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Leo kwako kesho kwa mwenzio

Na Barnabas Maro

**JAMBO** linalokupata leo liwe la shida au la raha huweza kumpata mwenzio kesho. Methali hii hutumiwa kutunasihi tusiwacheke wenzetu wanaokumbwa na matatizo kwa kuwa yanaweza kutukumba sisi pia.

Methali hii hutumiwa kumtanabahisha mtu aliyejitapa kwa kuwa na hali nzuri kesho huenda asiwe na hali hiyo na badala yake awe nayo mwenzake aliyemdharau.

Enyi wana wa jiji moja lililoitwa Bandari ya Salama mpo nami au tayari mioyo yenu imeanza kwenda kasi na kuwaweka katika hali ya wasiwasi? Hebu niwakumbushe kuwa "Liandikwalo ndilo liwalo." Maana yake jambo ambalo limeandikwa na Mungu ndilo linalokuwa.

Kwa uhalisia, jambo analojaliwa mtu ndilo limjialo, liwe baya au zuri. Huweza kutumiwa na mtu aliyefikwa na matatizo kujiliwaza.

Pia husemwa "Liandikwalo ndilo liwalo." Maana yake jambo ambalo limeandikwa na Mungu ndilo linalokuwa. Kwa hakika jambo analojaliwa mtu ndilo limjialo, liwe baya au zuri. Methali hii huweza kutumiwa na mtu aliyefikwa na matatizo kujiliwaza. Enyi maadui wa jadi mpo? Methali zote nilizoandika zawahusu nyie Simba na Yanga.

Kwa faida ya mashabiki wa Simba na Yanga ambao sio wanachama na ambao ndio wenye kiherehere (hali ya kuhamanika ya kutaka kutenda jambo fulani, hali ya kujiweka kimbelembele kutaka kueleza, kujua au kutenda jambo) wanapaswa kutambua jambo ambalo limeandikwa na Mungu ndilo linalokuwa.

Enyi viherehere mwapaswa kutambua kuwa "Liwapo lako ni jema, la mwenzio huwa baya." Maana yake tunakumbushwa kuwa bahati za watu hupishana.

Wenye 'chuki,' yaani hisia ya kutopenda kitu au jambo, ilhali 'chuki' ni kitendo cha mtu kutopenda mtu mwingine au kitu. 'Chukiza' kitendo cha kufanya jambo la kuudhi. Kitendo cha kiumbe kufika kiwango cha kutopendeza kwa wengine kutokana na matendo yake. Kwa kiasi kikubwa ndivyo walivyo mashabiki wa Simba na Yanga.

Ndivo walivyo mashabiki wa Simba na Yanga kwani wengi wao midomo yao imetawaliwa na wivu na chuki dhidi ya wapinzani wao. Ndio maana timu ngeni zinapokuja kupambana hapa nchini hupata msaada wa washangiliaji.

Hewaa! (Tamko la kukubali; hakika, sadakta). Wajinga ndio waliwao. Kwamba wajinga ndio wanaopumbazwa au kuliwa. Methali hii huweza kutumiwa kumpigia mfano mtu ambaye ameishia kudanganywa kwa njia inayoonekana kuwa rahisi sana. Jamani, hasa ninyi mashabiki wa Simba na Yanga mwapaswa kuzinduka kuwa:

"Upendo huvumilia, hufadhili; upendo hauna wivu, haujidai wala haujivuni. Upendo haukosi adabu; hautafuti faida yake binafsi, wala hauna wepesi wa hasira; hauweki kumbukumbu ya mabaya, haufurahii uovu, bali hufurahia ukweli. Upendo huvumilia yote, huamini yote; na hustahimili yote." (Ikorinto 13:4-7)

Leo jioni jua linapoendelea kuzama, Simba na Yanga zitashindania Ngao ya Jamii kwa mchezo utakaofanyika kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam. Ni mchezo wa kile kilichosemwa na wahenga kuwa: "fahari wawili hawakai zizi moja." Maana yake fahari wawili hawawezi kukaa zizi moja kwa kuwa kila mmoja atataka awe mkuu wa zizi na kwa hivyo watashinda wakipigana.

Methali hii hutumiwa kuelezea watu wanaoshindana au walio na uwezo sawa hawawezi kupatana au kusikilizana. Ndivyo walivyo mashabiki wa timu kongwe za Simba na Yanga ambazo zote zina vilabu vyao eneo la Kariakoo hapa jijini.

wa kawaida, kabla ya timu hizo kongwe kupambana uwanjani huwa na malumbano (majadiliano yenye hoja ambazo zinapishana kuhusu jambo, majibizano ya kushindana) kila upande ukitamba kuondoka na ushindi.

Kandanda ni mchezo unaochezwa kwa miguu, wenye timu mbili zinazoshindana. Kwa hiyo mchezo ni jambo ambalo watu au timu mbili hulifanya kwa kushindana ili kupata mshindi. Kuthibitisha hili, naomba timu itakayoshindwa iwape mikono na hongera wapinzani wao kwa sababu kufanya hivyo ni uungwana.

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

# TCB yajitosa kuinua wanawake kiuchumi

**Na Mwandishi Maalum,** MBEYA

BENKI ya Biashara Tanzania (TCB) imedhamiria kuinua hadhi ya wanawake kifedha kwa kuwawezesha kiuchumi na kuwasaidia kuwa wajasiriamali shupavu kupitia mikakati endelevu.

Hayo yalibainishwa jana mkoani Mbeya kupitia kongamano la pili la Wanawake na Biashara lililoandaliwa na TCB ili kuwasaidia wanawake kuzing'amua na kuzitumia fursa za kibenki kwa ajili ya maendeleo yao binafsi na kwa taifa.

Katika kongamano hilo benki hiyo iliwaeleza wanawake kuwa itatekeleza jukumu hilo adhimu kwa kuwa kinara wa huduma jumuishi za kifedha kwao.

Wakiongea kwenye kongamano hilo, maofisa wake waandamizi walisema mafanikio ya jitihada hizo yatatokana na mikakati ya TCB ya kufanya mapinduzi makubwa ya kuwahudumia wanawake.

Walisema benki hiyo itawaonyesha fursa zinazopatikana na kuwaelimisha namna ya kufanya biashara zenye tija.

Pia walisema njia suluhishi za kibenki zilizopo na mpya za kisasa zaidi zitatumika kumkomboa mwanamke kifedha na kumshirikisha kikamilifu katika ujenzi wa taifa.

Wataalamu hao walisema benki hiyo pia imejiandaa vizuri kwa hilo na kwamba iko imara kifedha na ina wigo mpana wa huduma na mtandao mkubwa wa kuzifikisha popote kwa wakati.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa benki hiyo, Sabasaba Moshingi, alisema wana mtandao wenye jumla ya matawi 82, miongoni mwake makubwa yakiwa 46 na madogo 36 ambayo yapo nchi nzima.

"Hapa Mbeya yapo matawi matatu na tunapanga kuyaongeza ili tuweze kuwahudumia vizuri zaidi," alibainisha.

Alisema mikutano kama hiyo itaandaliwa Zanzibar, Morogoro, Arusha, Mwanza na Dar es Salaam kwa lengo la kuwakutanisha wanawake kujifunza mambo mbalimbali na kuijua zaidi benki hiyo.

Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, alisema kongamano hilo limekuja wakati mwafaka ambapo watasaidiana na serikali kuhakikisha hakuna mwanamke anayeachwa nyuma kiuchumi na kimaendeleo.

"Kupitia mpango huu, TCB itatoa mchango mkubwa katika kubadilisha hadhi ya wanawake nchini kifedha na kiuchumi. Ninawapongeza kwa kuja na wazo hili, kwa hiyo wanawake wa Mbeya tuchangamkie fursa hii adhimu," alisema.

Aliitaka benki hiyo isitoe mikopo yake kiholela bila kuhakiki miradi tarajiwa na kutoa miongozo ya kuitumia mikopo hiyo vizuri.




Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson (wa pili kushoto), akimsikiliza mwalimu wa kituo cha watoto wenye uhitaji maalumu cha Child Support Tanzania kinachomilikiwa na mteja mjasiriamali wa Benki ya TCB, kabla ya kufungua kongamano la Mwanawake na Biashara, lililoandaliwa na benki hiyo, jijini Mbeya jana. Kushoto ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa benki hiyo, Sabasaba Moshingi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wabuni mbinu kuficha bidhaa feki

**Na Mwandishi Wetu,** KIGOMA

BAADHI ya wafanyabiashara wamebuni mbinu mpya ya kuficha bidhaa, ambazo zimepigwa marufuku katika Soko la Tanzania hasa vipodozi kama hatua ya kukwepa ukaguzi wa serikali.

Hayo yalisemwa jana na Ofisa Usalama wa Chakula wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Elisha Meshack wakati wa ukaguzi uliofanyika, mkoani Kigoma.

Alisema ukaguzi huo umefanyika kwenye maduka ya rejareja, jumla, kwa wasambazaji, maduka makubwa, migahawa na kwingineko, pia wametoa elimu kwa wananchi.

Ofisa huyo alisema wamebaini mbinu hizo, kwenye ukaguzi wa bidhaa sokoni katika Wilaya za Kasulu, Kibondo na Kakonko, mkoani Kigoma kwa lengo la kuhakikisha bidhaa zote zinazouzwa sokoni zinakidhi matakwa ya kiwango husika.

Alisema kuna wafanyabiashara wachache wasio waaminifu wanaoficha bidhaa zilizopigwa marufuku kwenye Soko la Tanzania hasa vipodozi kwenye mabegi yao ya mkononi au katika ndoo za kuwekea uchafu dukani na endapo mteja anatokea basi anapatiwa bidhaa hiyo kwa kificho.

Meshack alifafanua kuwa TBS haitasita kuchukua hatua stahiki kwa wote watakaobainika kuuza bidhaa zilizopigwa marufuku, kwani ni kinyume cha sheria.

Alisema kwa kuwa mbinu wanazozitumia tayari zimebainika, shirika hilo litahakikisha wafanyabiashara wachache wadanganyifu, ambao wanauza bidhaa za vipodozi vilivyopigwa marufuku kwa kificho wanachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

Ukaguzi huo, alisema ni sehemu ya mkakati wa shirika hilo, kusimamia vyema majukumu yake kwa kuhakikisha ubora wa bidhaa na kulinda afya na usalama wa Watanzania na watumiaji wote.

Wakizungumzia ukaguzi huo, wananchi wengi waliunga mkono hatua hiyo ya TBS ya kufanya ukaguzi na kutoa elimu kwa umma, kwa kuwa kitendo cha wafanyabiashara kuuza kwa kificho bidhaa zilizopigwa marufuku ni kielelezo, kuwa elimu imewafikia na wanajua kwamba wanavunja sheria.

"Tunafurahishwa na kazi inayofanywa na TBS kwani hata watumiaji wa bidhaa za vipodozi sasa hivi wanajua ni vya aina gani havitakiwi kwenye Soko la Tanzania. Tunawapongeza kwa kazi kubwa," alisema Joyce Edward, mkazi wa Kibondo.

Alisema ukaguzi huo utakuwa mwarobaini wa wafanyabiashara, ambao wamekuwa wakiuza bidhaa za chakula na vipodozi zilizokwisha muda wa matumizi na vilevile kuuziwa vipodozi vyenye viambata sumu.

Mwananchi mwingine aliyejitambulisha kwa jina la Naftary Elisha, alisema; "Naishukuru TBS kwa kufika kwetu kwani kwa kufanya hivi. Ninaamini sisi wananchi tutaepukana na udanganyifu wa wauzaji sababu wanachukulia udhaifu wetu wa kutojua mambo au kutosoma na kutuuzia bidhaa, ambazo hazina ubora na zilizokwisha muda wa matumizi. Nashauri jambo hili hili liwe endelevu, ili tabia hii ya udanganyifu kwa wananchi ikome kabisa," alisema.

# Vodacom yajivunia mtandao kupanuka

**Na Mwandishi Wetu**

KWA kushirikiana na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), Kampuni ya Vodacom Tanzania imepanua eneo la mtandao wake, katika maeneo ya vijijni na kuwafikia asilimia 92 ya wananchi na hivyo kujihakikishia nafasi yake ya uongozi katika utoaji wa huduma za mawasiliano nchini.

Uongozi wa kampuni hiyo, umebainisha kuwa teknolojia na uunganishwaji kimtandao, vina uwezo mkubwa wa kujenga jamii yenye usawa na ushirikishwaji kwa kuwezesha upatikanaji wa mtandao wa intaneti, ambao unawezesha ushiriki kiuchumi.

Kampuni hiyo pia, imejiwekea lengo la kufikisha uunganishwaji wa mtandao kwa kasi ya broadband kwa asilimia 65 ya wananchi, ifikapo mwishoni mwa mwaka huu na lengo la mwisho ni kufikia asilimia 90, ifikapo mwaka 2024.Hatua hii pia inaendana na lengo la serikali lililotangazwa la kuongeza uunganishwaji wa mtandao wa broadband kutoka asilimia 45 hadi kufikia asilimia 80. Hadi sasa, eneo lililounganishwa na Vodacom linawafikia asilimia 52 ya wakazi walio katika vijiji 1,184, nchini.

Taarifa iliyotolewa na uongozi wa kampuni hiyo kwa vyombo vya habari jana, ilibainisha kuwa kwa zaidi ya miaka 20, Vodacom Tanzania imekuwa ikiendelea kuwekeza na kuboresha mtandao wake, ili kuhakikisha kuwa inatoa huduma bora kwa wateja wake na kuwapatia teknolojia mpya na bidhaa za ubunifu. Kutokana na uwekezaji huo wenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 171.4, kwenye teknolojia ya 4G peke yake na kwamba Vodacom ina minara zaidi ya 3,000 yenye uwezo wa 2G, zaidi ya 2,800 ya 3G na zaidi ya minara 2,000 ya 4G.

Mkakati na sera za serikali ni zaidi ya kuwa na mtandao mpana tu bali kuhakikisha kuwa upatikanaji wa huduma hiyo ni wa haki na usawa kwa watu wake.

Upana wa mtandao wa Vodacom unaofikia maeneo yote ya nchi pia ni msingi wa utoaji wa huduma zinazookoa maisha kwa watumiaji walioko vijijini.

"Kwa ushirikiano na Hospitali ya CCBRT kwa mfano, zaidi ya wagonjwa 6,000 wa fistula wamepata huduma za upasuaji, wengi wao wakiwa wametokea vijijini," ilibainishwa katika taarifa hiyo.

Katika kuelekea kwenye jamii ya kidigitali, Vodacom Tanzania imejenga mtandao wa data wa kitaifa wenye kasi na wenye kuaminika unaowapatia watumiaji huduma za intaneti na kuongeza ushirikishwaji kwa jamii zilizotengwa na hata kusaidia kupunguza makali yatokanayo na mabadiliko ya hali ya hewa.

"Yote haya, ikiwa vilevile ni kampuni inayoongoza kwa kiwango kikubwa cha ulipaji kodi katika sekta nzima ya mawasiliano, ambapo katika kipindi cha mwaka 2015 hadi 2020 ililipa Sh. trilioni 1.9, ikiwa ni kodi kwa serikali," ilibainisha zaidi katika taarifa hiyo.

# Mgodi wafadhili wajasiriamali

**Na Mwandishi Wetu,** KASULU

WAWAKILISHI wa vikundi vya wajasiriamali kutoka vijiji vinayozunguka Mgodi wa Dhahabu wa Barrick Bulyanhulu ulioko katika Halmashauri ya Wilaya ya Msalala mkoani Shinyanga, wanashiriki maonyesho ya tatu ya wajasiriamali kitaifa yanayoendelea wilayani Kasulu kwa ufadhili wa kampuni hiyo.

Maonyesho hayo ambayo yatafikia tamati Septemba 30, mwaka huu, yakiwakutanisha wajasiriamali kutoka maeneo mbalimbali nchini, yameandaliwa na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kigoma na yalizinduliwa rasmi na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango.

Lengo la maonyesho hayo ni kutoa fursa ya kupanua wigo wa masoko ya bidhaa zinazozalishwa na viwanda vidogo, kubadilishana ujuzi na uzoefu kwa wanajisiriamali na wanaviwanda pamoja na kuonyesha teknolojia mbalimbali zinazozalishwa nchini.

Akizungumza kwa niaba ya wajasiriamali wenzake waliowezeshwa na Barrick kushiriki katika maonyesho hayo, Clementina Felix, anayejishughulisha na ushonaji na ubunifu wa mavazi, aliishukuru Barrick Bulyanhulu kwa kuwawezesha kushiriki maonyesho hayo makubwa ambayo yatawawezesha kujifunza mambo mbalimbali ili kukuza biashara zao.

"Kupitia maonyesho haya tutaweza kupata fursa ya kuonyesha bidhaa tunazozalisha, pia tutaweza kupata elimu ya kufungasha bidhaa, urasimishaji biashara na kufungua fursa zaidi za masoko, tumekuja na bidhaa zaidi ya 100 za kuonyesha," alisema Felix.

Aliongeza kuwa miongoni mwa wajasiriamali waliowezeshwa na Barrick, wanajihusisha na kilimo cha mazao ya nafaka, mboga na matunda, wafugaji wa kuku na nyuki, washonaji wa nguo na watengenezaji wa mazulia na viatu.

Ofisa Uhusiano na Jamii wa Mgodi wa Barrick Bulyanhulu, Antony Sebastian, alisema wajasiriamali hao ni sehemu ya shughuli za maendeleo ya Mgodi wa Bulyanhulu ambao wanawezeshwa kupewa elimu ya ujasiriamali na kwa wale wanaojishughulisha na kilimo wanapatiwa mbegu, mbolea na dawa za kuulia wadudu ili wafanikiwe kuendesha kilimo cha kibiashara.

Sebastian aliishukuru SIDO kwa kuandaa maonyesho hayo yaliyowakutanisha wajasiriamali na wadau mbalimbali wa sekta ya ukuzaji wa biashara ndogo.

## UHABA WATAALAMU

# Chuo cha Ardhi Tabora chapata dawa

**Na Mwandishi Wetu,** TABORA

UONGOZI wa Chuo cha Ardhi Tabora (ARITA) umesema kimepiga hatua kubwa ikiwamo kuongeza idadi ya wanafunzi ili kukabiliana na upungufu wa wataalamu wa ardhi nchini.

Umebainisha kuwa katika mpango kabambe wa miaka 10 (2010-2020) kimeongeza udahili mwaka hadi mwaka, idadi ya wanafunzi ikiongezeka kutoka wanafunzi 146 mwaka wa masomo 2009/2010 hadi kufikia 1,414 mwaka 2020/21.

Kaimu Mkuu wa Chuo hicho, Donald Rweramila (pichani) alisema jana kuwa tangu kilipoanzishwa mwaka 1979, kilikuwa kikiongeza udahili wa wanachuo kulingana na miundombinu iliyokuwapo.

Alibainisha kuwa mwaka 2009, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ilibuni mpango kabambe wa miaka 10 uliolenga kupanua chuo hicho kwa kuongeza miundombinu, kuongeza vitendea kazi ambavyo vilileta ongezeko la idadi ya wana chuo kutoka 146 mwaka 2009/10 hadi 1,414 mwaka 2020/21.

Kaimu Mkuu huyo wa Chuo alisema Chuo kimefanikiwa kuandaa na kuboresha mitaala yote kwa kufuata mfumo wa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) ili tuzo zitolewazo na chuo hicho ziwe na kiwango cha ubora unaokubalika kitaifa na kimataifa.

Alisema wamefanikiwa kupata usajili na ithibati kamili kutoka NACTE ya kutoa mafunzo ya Sekta ya Ardhi katika ngazi ya astashahada na stashahada.

"Wahitimu katika ngazi ya stashahada wenye ufaulu stahiki wanazo sifa za kujiunga na masomo ya shahada ya kwanza katika chuo kikuu chochote ndani na nje ya nchi kinachofundisha taaluma za Sekta ya Ardhi au zinazohusiana," alisema.

Aliongeza kuwa chuo pia kimeboresha mfumo wa upatikanaji wa maji safi kwa matumizi ya wanachuo katika bweni jipya kwa kujenga tanki la kuhifadhi maji chini ya ardhi lenye ujezo wa lita 200,000.

"Chuo kimeweza kuboresha mfumo wa umeme kwa kuingiza umeme wa njia tatu na kusimika transfoma ndani ya eneo la chuo ili kukidhi mahitaji ya ongezeko la matumizi ya umeme," alisema na kubainisha kuwa wamenunua jenerata kubwa lenye uwezo wa kuhudumia eneo lote la chuo wakati wa upungufu au hitilafu ya umeme unaotolewa na Shirika la Umeme (TANESCO).

Alisema chuo hicho pia kimefanikiwa kuanza ujenzi wa maktaba ya kisasa yenye uwezo wa kuchukua watumiaji 360 na kompyuta 50 kwa wakati mmoja.

"Chuo kimefanikiwa kusimika Mfumo wa udahili wa Wanafunzi ambao umebuniwa na kusimikwa na Chuo Kikuu Ardhi - Dar es Salaam.

"Mfumo huu shirikishi unasaidia kurahisisha usajili wa wanachuo, kutunza kumbukunbu sahihi za wanachuo, utangazaji wa matokeo ya mitihani na kudhibiti ulipaji wa ada za masomo kwa wanachuo," alisema.

Alibainisha chuo kimefanikiwa kuendelea kufanya ukarabati wa miundombinu mbalimbali iliyopo chuoni ikiwa ni pamoja na ofisi za watumishi, madarasa, mabweni ya wanachuo na unuzi wa samani.

Tangu chuo kilipoanzishwa mwaka 1979 hadi mwaka 2017, kimefanikiwa kutoa jumla ya wahitimu 3,303.



Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga, akizungumza na waandishi wa habari wa mkoa huo jana, katika kikao cha kufahamiana pamoja na kujadili maendeleo, ikiwa ni sehemu ya mpango wake wa kukutana na makundi mbalimbali wakiwamo wanahabari. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

# Wizara yavishtukia kikwazo sekta ya uwekezaji

**Na Mary Geofrey**

SERIKALI imesema inaendelea kuondoa vikwazo na urasimu usio na tija katika Sekta ya Uwekezaji ili kuendelea kuvutia wawekezaji wengi kuja nchini.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Uwekezaji, Geoffrey Mwambe, alibainisha hayo juzi alipozungumza na waandishi wa habari juzi mkoani Dar es Salaam.

Alisema katika kutekeleza hilo, watatumia njia mbalimbali ikiwamo kuondoa usumbufu katika kutoa vibali vya kazi hasa takwa la kuwalazimisha wawekezaji kuhakiki vyeti vyao kupitia Tume ya Vyuo Vikuu (TCU), Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) na taasisi zingine zilizokuwa zinachelewesha upatikanaji wa vibali.

"Kwa sasa vibali vinapatikana ndani ya muda mfupi na hata ndani ya siku moja," alisema Mwambe..

Alisema wizara hiyo inaendelea kuandaa waraka wa kubadili Sheria ya Uwekezaji nchini kwa ajili ya kuipeleka kwenye Baraza la Mawaziri wa Mapendekezo ya Kutunga Sheria Mpya ya Uwekezaji ya Mwaka 2021. Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha kunakuwa na sheria mpya ya uwekezaji na sera ya uwekezaji yenye mkakati wa utekelezaji ndani ya mwaka wa fedha 2021/22.

"Wizara inawashukuru wadau wote wa sekta ya umma na sekta binafsi kwa ushirikiano wao wa kutoa maoni na ushauri na inaendelea kuwaomba wadau watoe ushirikiano pale patakapohitajika," alisisitiza Mwambe.

Waziri huyo alisema wanaendelea kutekeleza majukumu ya uratibu wa uwekezaji nchini kwa mujibu wa Sera ya Uwekezaji ya Mwaka 1996 na Sheria ya Uwekezaji ya Mwaka 1997, ambazo zimetoa mfumo wa kuratibu masuala ya uwekezaji nchini.

Mwambe alisema wizara imeendelea kuratibu shughuli za maboresho ya mazingira ya uwekezaji na biashara nchini kwa kusimamia utekelezaji wa mpango wa mwaka 2010 wenye viashiria 11 vya wepesi wa kufanya biashara nchini.

Alisema pia wizara iliratibu ubainishaji wa vikwazo vya uwekezaji kwa kuwataka wawekezaji kuwasilisha vikwazo dhidi yao na ofisi yake ilipokea barua kutoka kwa kampuni 92 zenye hoja 106.

Alisema vikwazo hivyo vilihusu kunyang'anywa leseni ya mawasiliano, kuchelewa kwa umilikishwaji ardhi, marejesho ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), kuchelewa kutolewa kwa zabuni za kuzalisha umeme na kuchelewa kwa vibali vya Baraza la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (NEMC)

Vikwazo vingine ni kuzuiwa kufanya uendelezaji wa eneo la utalii, kuchelewa kwa vibali vya kazi, utaratibu wa uhamishaji wa hisa kwenye kampuni, utekelezaji wa kilimo cha mkataba na vibali vya ukazi.

"Ofisi inaendelea kushirikiana na wizara na taasisi zinazohusika kuhakikisha changamoto hizo zinafanyiwa kazi ipasavyo," alibainisha.

Kadhalika, alisema wanaandaa mwongozo wa wakuu wa mikoa na wilaya wa kutenga maeneo ya uwekezaji ambayo yamebainishwa kila kitu kwa ajili ya kutangazwa kwa ajili ya uwekezaji.

Kuhusu mafanikio ya wizara hiyo, alisema kuanzia Machi hadi Agosti mwaka huu, jumla ya miradi 133 imesajiliwa kulinganishwa na miradi 105 iliyosajiliwa katika kipindi hicho mwaka jana.

Alisema kupitia miradi hiyo, inatarajiwa kuzalisha ajira 29,709 kulinganishwa na ajira 8,252 zilizotarajiwa kuzalishwa katika kipindi kama hicho cha mwaka jana.



# Waziri aanika chanzo cha mgogoro

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, amesema kuwapo kwa mgogoro sugu wa wakulima na wafugaji Kata ya Malolo wilayani Mpwapwa kunasababishwa na viongozi kushindwa kupata suluhu.

Simbachawene aliyasema hayo juzi katika mkutano wa hadhara wa wananchi wa Kata hiyo, uliofanyika katika Kijiji cha Idodoma.

Kutokana na kubainika kwa chanzo hicho, alisema ni wajibu wa viongozi hao kutafuta suluhisho la mgogoro huo haraka iwezekanavyo.

"Kitendo cha mgogoro huu kuendelea kuwa sugu mpaka sasa na kutokupatikana kwa suluhu ni kuonyesha kushindwa kwa viongozi wa kata wakiongozwa na Ofisa Mtendaji wa Kata pamoja na viongozi wengine," alisema.

Simbachawene alimtaka ofisa mtendaji huyo kuhakikisha anafanya kikao cha mapatano kwa haraka kwa kukutana na Katibu wa Chama cha Wafugaji pamoja na wawakilishi wa wakulima na wafugaji ili kuzungumza na kumaliza mgogoro huo.

"Ukiona mfugaji anamchukia mkulima huyo hajitambui. Hatambui umuhimu wa mkulima kwa mifugo na ukiona mkulima anamchukia mfugaji hatambui umuhimu wa mfugaji kwa kilimo.

Nyie watu kwa asili mnategemeana, hivyo mnatakiwa kupanga utaratibu nyie wenyewe, si kuacha mtu anafanya anavyotaka. Lazima kuweka usawa maslahi ya watu hawa na hii ndiyo kazi ya viongozi," alisema Simbachawene.

Waziri huyo alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuidhinisha Sh. milioni 250 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kata ya Ipera, jimboni Kibakwe ambacho kikikamilika kitakuwa kinahudumia idadi kubwa ya wananchi kutoka katika kata mbalimbali zilizoko jirani na kata hiyo.

"Gharama ya ujenzi wa Kituo hiki ni Sh. milioni 500, lakini tayari Rais Samia ametoa Sh. milioni 250 ili ujenzi kuanza na pia nimejisikia na furaha baada ya kuwaona wananchi mkijituma kusafisha eneo hili litakalojengwa kitu cha afya.

Hakika mnaonyesha umoja wa hali ya juu, hongereni sana," alisema Simbachawene.

# Asilimia 20 ya Watanzania wana vinasaba vya ugonjwa selimundu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

TAKWIMU zinaonyesha kuwa asilimia 15 hadi 20 ya Watanzania wana vinasaba vya selimundu, imeelezwa.

Kutokana na hali hiyo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Prof. Abel Makubi, amewataka waganga wafawidhi katika hospitali za Rufani za mikoa nchini kuendeleza kampeni ya upatikanaji wa vifaa vya kupimia ugonjwa huo ili kukabiliana nao.

Akizungumza jana kwenye hafla ya kupokea vifaa vya kupimia ugonjwa wa selimundu vilivyotolewa na Taasisi ya General De Pharmacy Limited ya Mkoani Arusha, Katibu Mkuu huyo alisema jitihada zinahitajika ili kusaidia mapambano dhidi ya ugonjwa huo.

Prof. makubi alibainisha kuwa ugonjwa huo bado ni tatizo nchini na unachangia asilimia 6.7 ya vifo vya watoto chini ya miaka mitano.

"Natumani hizi mashine ambazo mnazipata ambazo zitaanzia katika hospitali za rufani zitashuka mpaka chini zitasaidia kukabiliana na ugonjwa huu," alisema na kuongeza kuwa gharama za upatikanaji wa mashine hizo ni kati ya Sh. milioni 300 na 400.

"Niwaombe waganga wafawidhi wa hospitali za rufani za mikoa na zile za wilaya kutoa 'support' (msaada) ya (wa) hii kampeni ya hivi vifaa ambavyo vitasaidia kupima mapema wagonjwa ambao wana sikoseli. Nitoe rai kwa wadau wengine wa maendeleo kuendelea kutoa misaada mbalimbali katika sekta ya afya ili kusogeza huduma za afya karibu na wananchi," alisema.

Prof. Makubi alisema anatamani kuwe na vituo vya kukabiliana na ugonjwa huo hususani kwenye mikoa yenye tatizo hilo na kuomba wadau wenye uwezo kusaidia jambo hilo.

Mkurugenzi wa General de Pharmacy Ltd, Neville Mushi, alisema vifaa walivyokabidhi vimegharimu Sh. milioni 28.

"Lengo la kukabidhi vifaa ni baada ya kusikiliza hotuba nyingi katika maadhimisho ya Siku ya Selimundu Duniani kuona kuwa tatizo hili ni kubwa sana nchini.

"Tulipokea maombi kutoka kwa Chama cha Selimundu Tanzania, wao walianza kuomba mashine mbili lakini kwa namna ya kipekee tulivyoguswa, tuliamua kuwapatia mashine tano pamoja na vipimo vya 'test' vya 50 kwa 50," alisema.

Pia alisema kipimo hicho hakitakuwa kikipima selimundu pekee bali kina uwezo wakupima magonjwa mengine pia kama maralia, virusi vya UKIMWI (VVU) na UVIKO-19.

Naye Mkurugenzi Msaidizi anayeshughulikia magonjwa yasiyo ya kuambukiza kutoka Wizara hiyo, Dk. James Kiologwe, alisema kwa sasa serikali ina vituo vitano ambavyo vinapima ugonjwa huo na wamejipanga kuhakikisha huduma ya upimaji inakuwa karibu na wananchi.

Alisema kila mwaka watoto 11,000 wanazaliwa wakiwa na tatizo la ugonjwa huo.

"Kwa hiyo tunataka huduma hizi zifike karibu na wananchi, cha kufanya ni kuhakikisha vifaa vinafika hii ni chachu tu kuonyesha katika hospitali zetu ni rahisi kuwafikia lengo letu ni kuhakikisha watu wengi zaidi wanapimwa kama wanavinasaba vya ugonjwa wa selimundu," alisema.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu akizungumza wakati wa kufungua kikao kazi cha wakurungenzi wa mamlaka za seikali za mitaa, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Ummy azindua mwongozo wa miradi mkakati

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, amezindua mwongozo wa uandaaji wa miradi ya kimkakati itakayosaidia kuanzisha na kuendeleza miradi inayozalisha mapato kwa serikali za mitaa.

Mwongozo huo umeandaliwa kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Mitaji (UNCDF) na ulizinduliwa jana jijini hapa kwenye mafunzo kwa Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Waziri Ummy alisema mwongozo huo umeakisi mpango wa taifa wa maendeleo wa miaka mitano na itasaidia halmashauri kubuni miradi itakayoongeza mapato ya halmashauri.

"Tunashukuru sana wadau wetu kwa kuendelea kuwa nasi kwenye shughuli mbalimbali za uwekezaji kwenye mamlaka za serikali za mitaa," alisema.

Pia alisema serikali iko kwenye maboresho ya uwekezaji ambapo inatarajia kuanzisha idara ya viwanda, biashara na uwekezaji katika mamlaka hizo.

"Hatutaki mbaki kwenye kukusanya tu mapato tunataka kuona kitu gani kimechochea uchumi katika eneo lako, kwa hiyo hii inasubiri ngazi ya mwisho ya Rais lakini hatua zote muhimu zimepita," alisema.

Kadhalika, alisema katika mwongozo wa kupata fedha za miradi ya kimkakati ameomba Wizara ya Fedha na Mipango kupitia upya kwa kuwa unabeba sana Halmashauri zenye mapato makubwa na kuacha zisizo na mapato.

Awali, Mkurugenzi wa UNCDF, Peter Malika, alisema shirika hilo limekuwa likifanya kazi na serikali kwa kushirikiana na TAMISEMI sehemu mbalimbali kwenye mitaji ya maendeleo na miradi ya kimkakati.

"Kuna Halmashauri takribani 20 ambazo tumefanya uwekezaji pamoja kwenye miundombinu ikiwamo stendi ya mabasi, masoko, redio za kijamii."

"Kuna miradi mingine inajengwa na mingine imeshakamilika na inafanya kazi kwa hiyo kuhusu mwongozo wa kutengeneza bankable project ni sehemu ya miradi ya mikakati,"alisema.





# China yaipiga jeki Zanzibar elimu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAKATI Zanzibar inaadhimisha miaka 57 ya elimu bila malipo, serikali ya China inatarajia kutoa vifaa mbalimbali kwa ajili ya kusaidia sekta ya elimu visiwani hapa.

Akizungumza jana na Nipashe, Balozi Mdogo wa China aliyepo Zanzibar, Zhang Zhisheng, alisema China imeamua kuiunga mkono Zanzibar katika kusherehekea siku ya elimu bila ya malipo ambayo lengo lake ni utoaji wa elimu bure kwa watu wote.

Balozi Zhang alisema vifaa hivyo watakavyovitoa ni pamoja na kompyuta, mashine ya uchapaji nyaraka, na vifaa vingine vya maabara kwa Shule ya Ufundi Kengeja, Pemba na Shule ya Ufundi Mikunguni, Unguja ili kurahisisha upatikanaji wa elimu.

Alisema vifaa hivyo wanatarajia kuvikabidhi kwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Muhammed Said, hivi karibuni ili kuvisambaza kwa shule hizo.

"China na Zanzibar ni marafiki wa karibu sana, hivyo serikali ya China itaendelea kuisaidia Zanzibar na Tanzania kwa ujumla katika harakati mbalimbali za maendeleo," alisema Balozi Zhang.

Balozi huyo alisema vifaa hivyo vitawasaidia wanafunzi wa shule hizo za ufundi kuboresha ujuzi wao na kufaulu vizuri katika mitihani yao.

Akizungumza katika maadhimisho ya miaka 57 ya elimu bila malipo, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, alisema Taifa haliwezi kusonga mbele bila kuwapo mipango na sera makini katika sekta ya elimu inayolenga kuiwezesha na kuiongoza jamii kuelekea maendeleo ya kweli.

Rais aliyasema hayo juzi katika hotuba yake iliyowasilishwa na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, katika kilele cha maadhimisho ya miaka 57 ya sherehe ya elimu bila malipo, zilizofanyika katika Kiwanja cha Gombani, Pemba.

Alisema Mapinduzi ya Januari 1964, chini ya Jemedari Hayati Mzee Abeid Amani Karume, yalilenga kumjengea uwezo Mzanzibari na kumkomboa kila mwananchi wa visiwa vya Unguja na Pemba kiuchumi na kimaendeleo kupitia uwekezaji katika sekta ya elimu.

Dk. Mwinyi alisema nia ya dhati ya serikali ni kuendeleza matunda ya Mapinduzi ambayo ni pamoja na kumpatia kila mtoto elimu bure na kumwezesha katika kukabiliana na ushindani wa soko la ajira duniani na Zanzibar ikiwa sehemu ya dunia inayohitaji kwenda sambamba na kasi ya mabadiliko.

Katika utekelezaji wa azma hiyo, Rais Dk. Mwinyi alisema serikali ya Zanzibar imekuwa ikishirikiana na wadau mbalimbali wa elimu ili kuleta tija na mabadiliko katika sekta ya elimu nchini.

Alisema kuna ongezeko kubwa la mahitaji ya mikopo ya elimu ya juu kwa wanafunzi wenye sifa. Jumla ya Sh. 11,105,850,239 zimetumika kwa mwaka 2019/20 kuwapatia mikopo wanafunzi 4,040 wakiwamo wapya na wanaoendelea na masomo.



Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Muhamed Said (kushoto), akizungumza na Balozi mdogo wa China Zanzibar, Zhang Zhisheng (katikati), ofisini kwake, Mazizini Unguja jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Polisi kuchunguza mauaji ya kikatili

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JESHI la Polisi Zanzibar limesema linaendelea kufanya uchunguzi wa mauaji ya kikatili yaliyotokea mwanzoni mwa wiki hii Kianga, Wilaya ya Magharibi Unguja.

Katika mauaji hayo, mama mwenye umri wa miaka 23 alidaiwa kuuawa kikatili kwa kupigwa na kitu chenye ncha kali.

Mtu huyo aliyetambuliwa kwa jina la Zulfa Sheghan, mama wa mtoto mmoja, alikutwa amefariki dunia nyumbani kwake Kianga, majira ya saa 2:30 asubuhi, akiwa utupu huku dunia akiwa na majeraha makubwa mwilini mwake.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi, Awadhi Haji Juma, alisema bado jeshi hilo linaendelea na uchunguzi wa tukio hilo na kwamba linahitaji umakini mkubwa katika upepelezi wake.

Alisema Zulfa alikutwa ameshafariki dunia nyumbani kwake huku mwili wake ukiwa unachuruzika damu kutokana na majereha makubwa aliyokuwa nayo mwilini.

"Tunaendelea kuwashikilia baadhi ya watu kwa uchunguzi zaidi kuhusu mauaji haya ya mama huyo ambaye ameacha mtoto mdogo mwenye umri wa mwaka mmoja," alisema Kamanda Awadh.

Sheha wa Shehia ya Kianga, Juma Issa, alisema tukio hilo lililotekea katika shehia yake limeleta taharuki na tishio kubwa kwa wananchi wa shehia hiyo.

Alisema tukio kama hilo la kikatili halijawahi kutokea katika shehia hiyo, hivyo aliliomba jeshi la polisi kufanya uchunguzi wao ili kuwabaini waliohusika na tukio hilo.

# Uwasilishaji wa michango ZSSF sasa kidijitali

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

UWASILISHAJI wa michango ya wafanyakazi wa serikali na taasisi zake pamoja na mashirika binafsi katika mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) kuanza kutumika kwa mfumo wa kielektroniki.

Kutokana na mfumo huo mpya, maofisa wanaohusika na uwasilishaji michango hiyo, wametakiwa kuwa na ushirikiano kwa kuupokea na kuuzoea mfumo huo ili taarifa za waajiriwa ziendane na michango wanayoitoa

Mkurugenzi wa Uendeshaji na Utumishi, Juma Ali Simai, aliyasema hayo jana wakati akifungua mafunzo yaliyowashirikisha maofisa utumishi, wahasibu na maofisa Teknolojia ya habari na Mawasiliano (TEHAMA) wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na taasisi zake kuhusiana na uwasilishaji michango kwa njia ya kielektroniki.

Mafunzo hayo yalifanyika kwenye ukumbi wa mkutano wa Wizara hiyo, Migombani, Zanzibar.

Aliwataka washiriki hao kufahamu kuwekwa kwao pamoja katika mafunzo hayo ni kujengewa uelewa na kuzidisha uwezo katika majukumu yao kwa kushirikiana jambo ambalo litatoa fursa kwa watendaji kusaidiana pale ambapo kutatokea mabadiliko iwe ya kubadilishwa ofisi au ya kiutendaji

Pia aliwataka kukaa na watumishi wote na kuwapa elimu kwa walichojifunza na hakuna sababu ya mfanyakazi yeyote wa ofisi hiyo kubaki nyuma au kupitwa na mfumo huo kupitia simu za kiganjani au kompyuta ili kila mmoja aone kama kuna upungufu au kukosekana taarifa sahihi za michango yake.

Juma alisema Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais itaendelea kutoa mafunzo kwa watendaji wake na taasisi zake kwa kila kada kila hali inaporuhusu na kwa mujibu wa mpango mkakati wa ofisi hiyo.

Naye Meneja TEHAMA wa ZSSF, Ali Haji Ameir, alisema mafunzo ya kujenga uelewa ni muhimu ikizingatiwa kuwa ZSSF imejipanga vyema na itakapofika Desemba, mwaka huu, itakuwa mwisho wa uwasilishaji michango kwa njia ya kawaida iliyozoeleka.

Alisema badala yake taasisi za serikali na mashirika binafsi yatawasilisha michango ya wanachama kwa njia ya kielektroniki.

Alisema njia ya kisasa ya mfumo wa kielektroniki ya uwasilishaji michango ya wanachama wa ZSSF ni rahisi na salama zaidi iwapo mwasilishaji atakamilisha taratibu za usajili.

Washiriki wa mafunzo hayo wamejifunza jinsi ya kuwasilisha michango ya wafanyakazi kwa ZSSF, maslahi ya watendaji kuelekea kustaafu, namna ya mwanachama mmoja mmoja wa mfuko kupata taarifa kwa kutumia simu ya kiganjani au kompyuta.



## WABABE WAMEUMANA

# Diamond, Ali Kiba, Harmonize meza moja

WABABE wa muziki wa Bongo Fleva, hatimaye wamekutanishwa katika meza moja, iwe isiwe anatakiwa mmoja wao kuibuka mshindi.

Wasanii hao, Diamond Platnumz, Ali Kiba na Harmonize, wamewekwa katika kundi moja la kugombea tuzo ya Afrima ambayo zitatolewa Novemba nchini Nigeria.

Katika orodha iliyotolewa Jumatano, Tanzania imefanikiwa kuingiza wasanii wengi kuliko miaka ya nyuma na hivyo kuonyesha muziki wa Bongo Fleva unavyozidi kuimarika.

Kipengele ambacho kitawakutanisha wababe hao ni kile cha Mwanamuziki Bora wa Kiume, ambapo kinawaniwa na kibao cha Waah (Diamond fit Koffi Olomide, Proud of You (Darassa fit Ali Kiba), Attitude (Harmonize fit Awilo Longomba & H baba) na Kalebe (Rayvanny akimshirikisha Inoss'B).

Kwa upande wa Diamond wimbo wa Waah! ndio umembeba, kwani licha ya kumuingiza katika vipengele vinne pia umetajwa katika vipengele saba vikiwemo wimbo bora wa mwaka, video bora ya mwaka, wimbo unaochezeka na wimbo bora wa kushirikiana.

Wanamuziki wengine walioteuliwa kuwania tuzo hizo ni Nandy (Number one) ulioingia katika kipengele cha Muziki Bora Afrika wa Kushirikishwa, Rosa Ree (Satan) Muziki Bora wa Hip Hop na Zuchu (sukari), Mwanamuziki Bora Anayechipukia

BASI SAWA

## Maua kuchanua kimataifa

MWANAMUZIKI  Maua Sama, ameamua kuvuka mipaka na safari hii anakuja na ngoma yake mpya aliyomshirikisha mkali kutoka Marekani T Pain.

Hivi karibuni Maua aliachia wimbo wake unaotamba kwa sasa "Away" ambao amempa nafasi rapa Young Lunya, kufanya vitu vyake.

Maua ambaye amerejea katika muziki, baada ya kupona matatizo yake ya kiafya yaliyokuwa yakimsumbua kwa takribani nusu mwaka.



## Nyota Shine kutikisa Jiji la Mwanza

MWIMBAJI wa Injili kutoka Mbeya, Bahati Simwiche, ameweka wazi lengo la kufanya tukio kubwa la kuadhimisha miaka mitatu ya huduma yake ya Nyota Shine, itakayofanyika jijini Mwanza.

Akizungumza na BT, Bahati amesema tayari waimbaji wengi wamethibitisha kupanda jukwaani Oktoba 10, mwaka huu katika Kanisa la Pentecostal Worship Center Canaan TZ ( NATA).

"Mbali na kufanya kumbukumbu ya miaka mitatu ya huduma ya Nyota Shine, pia itaambatana na kumbukizi ya kuzaliwa kwangu, hivyo wakazi wa Mwanza wajitokeze kwa wingi, kwa sababu kutakuwa na waimbaji wengi na tutaanza saa 8 mchana," amesema Bahati.





## 'Makomando Day' ya Masanja kupamba kesho

VIJANA wa  Kanisa la Feel Free linaloongozwa na mchekeshaji Emmanuel Mgaya, maarufu kama Masanja Mkandamizaji, kesho wanatarajia kunogesha kilele cha wiki ya makomando wa Yesu.

Akizungumza na BT, kiongozi wa vijana hao, MC Jo amesema lengo lao ni kutaka kuonyesha jamii upendo wa Mungu na kujitoa kwenye jamii.

"Tumekuwa na wiki ya kufanya shughuli mbalimbali za kijamii, kama Makomando Team katika Jiji la Dar es Salaam na kesho tutakuwa na kilele pale kanisani Feel Free Church Leaders Club Kinondoni, kuanzia saa nne mpaka saa nane mchana na chakula kitakuwa ni bure kwa wote," amesema MC Jo

## Mali ya urithi: Tamaa inavunja undugu

**Na Adam Fungamwango**

SIKU zote mali ya urithi kama ndugu mna akili za kushikiwa, basi mnaweza kugombana na kukataana undugu. Wazazi wanapofariki hasa wenye uwezo na kuacha mali nyingi, familia inabidi mkae kwa amani na kuangalia nini cha kufanya kuzitunza au kuziendelea. Lakini kama kuna kundi au mmoja akataka yeye ndiye awe juu, au mmliki, basi mali hiyo inaweza kugeuka kuwa balaa na chanzo cha matatizo makubwa.

Hapa leo tunaiangalia filamu ya 'Mali ya Urithi' Inazungumzia kuhusu mtu anavyoweza kuwa na uchu wa mali ambayo hajaichuma. Ni mali ya urithi, lakini anataka kumiliki pekee kama yeye ndiye mtoto pekee wa marehemu, kumbe ana ndugu zake.

Imechezwa na wasanii, Issa Juma, Hassan Hamza, Fatuma Makame, na wengineo.

Inaanza kwa kumwonyesha Bambucha akigombana mdogo wake kuhusu mali za marehemu baba yao. Haji alikuwa anataka mgawo wa marehemu baba yao na yeye aupate. Bambucha ambaye amechangia baba tu na Haji, lakini mama mbalimbali, aliakuwa akikataa. Haji hakuwa na kipato kikubwa, huku Bambucha akiwa amehodhi mali yote.

Wakati Haji akipigania kupata mgawo wake, Bambucha akatafuta majambazi ili wamuue mdogo wake. Lengo ni kuondoa bugudha na amiliki mali kwa amani na autuliu. Alikuwa anaungwa mkono na mkewe. Lakini mabinti wawili wa Bambucha akiwemo Eva walipinga, lakini hakuwa na la kufanya.

Pablo, alilongoza kundi watu wengine wawili. Hata hivyo pablo alitumia akili. Alitaka Haji akamatwe na kuwekwa getoni kwao kwa sababu hawakumwamini sana Bambucha kama anaweza kutoa pesa. Pili walishajua lengo la Bambucha ni kutaka kumdhulumu mdogo wake mali. Wakamchukua na kumhifadhi getoni kwao. Wakamdanganya Bambucha kuwa tayari wamehamuua Haji. Sasa akaanza kuwapiga chenga pesa yao. Wakagundua kuwa ni kweli hata wangemuua Haji wasingepata pesa. Pablo alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na mtoto wa Bambucha, Eva. Kwa ajili ya mapenzi, alimpa siri kuwa baba yao ana mpango wa kuwaua, ili kuficha siri ya wao kumuua Haji. Pablo na wenzake nao walikuwa na nia ya kumuua Bambucha. Hapo ndipo moto unapowaka. Pablo na vijana wake wawili, wakiungana na Haji wakavamia nyumbani kwa Bambucha na kumuua familia nzima, kasoro Eva. Eva naye akalipiza kisasi cha kuuawa wazazi wake, kwa kumuua mpenzi wake Pablo. Kabla hajaendelea kuua wengine akiwamo Haji, anakamatwa na polisi.







## Barnaba ajitetea kuvaa sketi

**Na Kalebo Mussa, TUDARCo.**

MSANII wa Bongo fleva, Elias Barnaba maarufu kama 'Barnaba Classic' ameweka wazi  kuhusu kusambaa kwa picha mbalimbali katika mitandao ya kijamii, zikimuonesha akiwa amevaa sketi.

Amesema  sababu ya kuvaa vile kuna kitu kikubwa kinakuja mbele, hata hivyo hapati shida na watu wanaomshutumu kuvaa nguo hiyo.

"Nilivaa sketi kwa sababu kubwa sana, waliosababisha nivae ile sketi wamenipa pesa nyingi" alisema Barnaba.

Aidha, Barnaba alisema kuwa vazi lile linaitwa Baji makaa,  ambapo askari  wa kikoloni walikuwa wanavaa, Wahindi wekundu wanavaa ndiyo  sale zao, Uturuki  pia wanalitumia vazi hilo.

## MSHENGA ALIVYOMTAPELI KING MAKUSA

**Na Adam Fungamwango**

KATIKATI ya mwezi huu, Tanzania ilipata pigo la kuondokewa na mwanamuziki nguli, Juma Ubao ambaye alijulikana kwa jina la King Makusa.

Alifariki dunia na kuzikwa Kisutu jijini Dar es Salaam. Anakumbukwa kuwa alikuwa kiongozi wa bendi ya Biashara Jazz, Six Manyara na hata bendi ya Tanzania All Stars, ambayo ilikuwa ni kama Taifa Stars kwa upande wa soka, ikikusanya wanamuziki kutoka bendi mbalimbali na kuunda bendi iliyokwenda kurekodi nyimbo nne kali, kwa ajili ya taifa, kuhamasisha uzalendo na kuomboleza kifo cha Samora Machel wa Msumbiji.

Alipewa jina la King Makusa, ikiwa ni kifupi cha jina la King Makusanya, kutokana na umahiri wake wa kupiga vyombo vingi kwa wakati mmoja.

Atakumbukwa kwenye miaka ya katikati ya 1970 hadi katikati ya miaka ya 1980, alitoa vibao vingi vikali akiwa na bendi ya Biashara Jazz ambavyo leo katika kumuenzi tutavitazama.

Na karibuni nyimbo nyingi alizotunga zilikuwa za matukio ya kweli kwa mujibu wa yeye mwenyewe akiwa hai.

**Posa Nitaleta**

Ni wimbo alioutunga kutokana na kutapeliwa pesa na rafiki yake, ambaye alimpa kazi ya ushenga, yaani kupeleka posa kwa wazazi wa msichana aliyetaka kumuoa.

Jamaa hakupeleka posa na akamkataa Makusa kuwa hajampa pesa. Pamoja na kupelekwa polisi na mahakamani, mshenga aling'ang'ania msimamo wake, kuwa hakupewa kitu. Na cha zaidi alishinda kesi. Ilibidi Ubao atafute pesa zingine, ili apeleke kwa wazaa chema. Kutokana na hasira alizokuwa nazo akatunga kibao hicho, ambacho kiliondokewa kuwa maarufu sana mwanzoni mwa miaka ya 1980.

**Kipini cha dhahabu**

Wakati akiishi nyumba za kupanga, alikutana na kisa cha akinamama wakiwa wanamshawishi mwenzao kutafuta mabwana.

Wanawake wa nyumba hiyo, baadhi wakiwa ni wake za watu, walikuwa wakimkoga mwenzake mmoja, ambaye alikuwa havai nguo nzuri, pia hata chakula alichokuwa akipika kilikuwa ni duni.

Wenzake wakawa wanamwambia asiwe mjinga, atakula dagaa kila siku, atafute bwana. Hilo lilimsukuma kutunga wimbo huo kuwaonya.

**Thamini Chako**


Wimbo huu aliutunga baada ya kushuhudia demu wa rafiki yake akivuliwa nguo mbele za watu. Ubao aliongozana na rafiki yake huyo aliyekuwa na mpenzi wake, wakielekea kwenye muziki. Ghafla wakavamiwa na akinadada watatu, wakaanza kumvua nguo demu wa rafiki yake. Kwa bahati nzuri baadhi ya akinamama wakamsitiri msichana yule. Ndipo ilipobainika kuwa alikuwa ameazima nguo. wakati ule kuazima nguo, hasa kwa akinadada ilikuwa ni jambo la kawaida sana.

**Ondoka Kaburu**

Hakuwa nyuma kwenye nyimbo za siasa. Wakati kukiwa na harakati za ukombozi Kusini mwa Afrika, nchi nyingi zikiwa hazijapata uhuru ikiwamo Afrika Kusini, King Makusa alitunga wimbo wa 'Ondoka Kaburu'.

**Maduka ya Ushirika**

Mwanzoni mwa miaka ya 1980, hasa baada ya vita ya Kagera, nchi iliingia kwenye hali ngumu ya uchumi. Ndipo yalipoanzishwa maduka ya ushirika, ili kupunguza adha ya njaa. Wanamuziki hawakuwa nyuma kupigia debe uanzishwaji huo. Juma Ubao naye akawa mmoja wao.






# Wizkid azidiwa upweke

MWANAMUZIKI nyota kutoka Nigeria, Ayodeji Balogun, maarufu kama Wizkid, sasa ameanzisha vita na warembo, baada ya kutangaza yupo katika mchakato wa kutafuta mke.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Wizkid, amesema amekuwa baba na mlezi pekee, sasa ni muda wa kuwa na mke, ambaye atawajibika, akiwa katika ziara zake za muziki.

Nipo peke yangu kama baba, natumaini kutafuta mke katika ziara yangu hii," ameandika Wizkid.



## Tonto, Prince mambo magumu

MGOGORO kati ya mwigizaji kutoka Nollywood, Tonto Dikeh na mpenzi wake wa zamani Prince Kpokpogri, bado unazidi kupamba moto, baada ya kufikishana kortini.

Hata hivyo, Prince, amewasilisha zuio la kuitwa mahakamani katika Idara ya Ustawi wa Jamii (DSS), akitaka haki ya msingi ifuatwe.

Mwigizaji huyo, amefungua shauri hilo mahakamani akidai talaka akilalamika aliyekuwa mume wake ni msaliti, mlafi na kupata mali kwa uongo.

## BBNaija-2021 Saga alaumiwa kuwa mbumbumbu kimahaba

WAKATI shindano la Big Brother Nigeria (BBNaija) likizidi kuchanja mbuga, baadhi ya mashabiki wameanza kuwalalamikia washiriki kufanya vitu kwa majaribio.

Moja ya tukio lilowaudhi mashabiki hao ni kitendo cha kuvunjika ghafla uhusiano wa kimapenzi kati ya Saga na Nini, ambao ulikuwa ukifuatiliwa na wengi.

Mwimbaji Orezi, amejiunga na watu wanaolalamika kwa kueleza penzi hilo kufa ghafla limepoozesha shindano hilo.

"Saga anajishughulisha na mpenzi wa mtu mwingine, ambaye hatumii fursa yoyote kumjulisha juu ya mapenzi yake kwa mpenzi wake. Yupo kama mtoto mchanga kwenye Runinga anatia aibu mbele ya watazamaji milioni 90 " ameandika katika akaunti yake ya Instagram.





## Rita siku zote hukuwaonyesha sukari yako?

MASHABIKI wa mwigizaji wa Nollywood, Rita Dominic, amepata mshangao baada ya msanii huyo, kutoka matembezini na mume wake, Fidelis Anosike, jambo ambalo halikuwahi kutokea.

Wawili hao wameonekana wakiwa pamoja katika hafla moja iliyofanyika wiki iliyopita mjini Logos na kusababisha watu kuwa na shauku kubwa.

"Kila kitu kinakuja kwa wakati wake, Mungu wangu hakuna jambo la kushangaza ni mapenzi yetu kutoka wawili leo," amesema Rita.

## Moneybagg sasa hiyo sifa

UNAWEZA kusema ni kichaa cha pesa, lakini kwa rapa maarufu wa Marekani, Moneybagg Yo, anaona ni jambo la kawaida kwake hasa katika kuonyesha ukwasi wake wa kifedha.

Juzi mwanamuziki huyo, alisherehekea miaka 30 ya kuzaliwa kwake kwa kuanika msururu wa magari anayomiliki, ikiwamo malori mawili mapya ya mizigo yaliyopakiwa katika meli yake kubwa.

Rapa huyo anayesifika kwa kutembea na pesa nyingi wakati safari zake, zilizo na gharama kubwa.

Moneybagg Yo, aliweka picha katika ukurasa wake wa Instagram kuonyesha meli yake hiyo, iliyosheheni magari ya kifahari yenye rangi nyekundu.



MAKALA

# Ndivyo mboga za majani za asili zilivyosheheni dawa na viini lishe

## ●Ni mgagani, mnafu, mlenda, kinga maradhi mlipuko

**NA MWANDISHI WETU**

UNAPOZUNGUMZIA mboga za majani za asili si wote wanaofahamu mboga za asili zenye virutubisho vingi na viini lishe muhimu vinavyoboresha afya zao.Japo huliwa kama mboga na kuongeza virutubisho, utafiti umebaini kuwa pia ni dawa zinazotibu maradhi mbalimbali.

Mboga za mgagani, mnafu, mchicha wa kienyeji, mlenda, bamia za kienyeji na nyanya chungu zina virutubisho na viini lishe vingi kwa watu lakini pia ni tiba.

Kwa mfano mgagani na mnafu, zinasaidia watu waliotumia dawa za hospitalini kwa wingi, zinaweza kusafisha 'takasumu' za dawa zinazobaki mwilini baada ya mgonjwa kutumia tiba kwan muda mrefu, wakati nyanyanchungu hudhibiti shinikizo la juu la damu.

Ni maelezo ya Ofisa Lishe wa Shirika la MIICO, Anna Minja, linalofanya kazi zake katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini , aliyoyatoa kwa wanahabari na ujumbe wa shirika laActionAid Tanzania, katika ziara ya kutembelea miradi inayofanywa na mashirika hayo ikiwamo kuboresha lishe ya familia, kukabiliana udumavu na kuinua uchumi wa wananchi kwenye mikoa hiyo.

Anasema MIICO kupitia program ya kujenga kilimo shirikishi na shindani cha mboga na matunda Nyanda za Juu Kusini, inawafundisha wakulima wadogo katika Wilaya ya Mbozi Mkoa wa Songwe kulima mboga za asili na matunda ili kuboresha lishe za wanavijiji.

Anaongeza kuwa mboga za asili zimesheheni madini na vitamini nyeti kama, vitamin A, inayoongeza kinga mwilini na nguvu ya macho, folic acid iliyo muhimu kuzalisha damu na kujenga mfumo wa fahamu-ubongo na uti wa mgongo.

Zina vitamin C inayohitajika kutibu na kuponya seli zilizoumia. Ndani ya mboga hizo kuna madini mfano zink ambayo ni muhimu kuimarisha kinga ya mwili, hasa enzi hizi za magonjwa yanayoambukiza, pia zina utajiri mkubwa wa virutubisho.

"Katika zama hizi za mabadiliko ya tabianchi ni himilivu na zina uwezo wa kukabiliana na madiliko ya hali ya hewa , ikilinganishwa na mboga zinazozalishwa kwa mbegu za kisasa kutoka nje," anaongeza.

Ofisa huyo anasema wanawajengea uwezo wa kuzalisha vyakula vyenye lishebora pamoja na kufanya kampeni mbalimbali ili kuwa na ulaji wa mboga na matunda kuboresha afya na lishe kwa wananchi, kupunguza udumavu miongoni mwa watoto.



Mkulima Flora Mlowezi ni mzalishaji mbegu za asili akiwa shambani kuvuna mbegu za figiri au roshu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Anasema ili mradi huo uwe endelevu wanawafundisha wakulima kuzalisha mbegu za asili, kutumia mbolea za asili kama mboji na samadi na viuatilifu vya asili kukabiliana na wadudu wavamizi yote yakihakikisha ubora na usalama wa chakula katika mikoa wa Songwe, Mbeya, na Katavi.

Anasema ili kusaidia wakulima wadogo wanawake, MIICO inashirikiana na wadau kuwafunza utaalamu wa kuzalisha mbegu za mboga za asili na kuwauzia wakulima wengine vijijini na kwamba wilayani Mbozi wanafanyakazi katika kata za Mahenge na Igamba.

Anataja mbegu za mboga za asili zinazozalishwa kuwa ni mgagani, mchicha, mnavu na bamia na lengo la mradi ni kuboresha lishe ya wanafamilia vijijini na kupunguza udumavu na maradhi, kukuza uchumi wa wakulima wadogo hasa wanawake na kuondoa umaskini.

Anna anasema, katika maeneo hayo kila kaya inahamasishwa kuwa na bustani ya nyumbani wakati wa mvua, lakini pia inayonyweshewa kwa kutumia maji yanayotumiwa nyumbani wakati wa kiangazi. Aidha inayotumia mbolea na viuatilifu vya asili kwenye uzalishaji.

**KUZALISHA MBEGU**

Akizungumzia kuzalisha mbegu za asili anasema wanashirikiana na Shirika la World Vegetable Centre lililoko Arusha, na wakulima wadogo wanawake wazalishaji hupewa mbegu 'basic seeds' au mbegu mama.

"Hizi huoteshwa ili kutoa mbegu. Hawazichumi. Na mashamba yanayootesha ni lazima yatengwe mbali yasiwe karibu au kuzungukwa na mazao kama hayo. Mbegu zikikomaa wanazikausha na kutambuliwa kwa jina kama ni bamia, ngogwe au mchicha na hufunganya kwenye paketi na kuuzwa kwa wakulima wengine." Anasema Anna.

Aidha, wanawafundisha kuzipanda, kuzitunza kwa mfano mchicha hupandwa moja kwa moja shambani lakini ngogwe hupandikizwa kwanza kwenye trei zikishaota na kufikia kimo kinachokubalika huhamishiwa shambani au bustanini na kustawishwa, anasema.

Je, mbegu zinazolimwa Mbozi zinaweza kutumika sehemu nyingine nchini? Anna anasema hapana. Kwa mujibu wa sheria ya uhakiki na ubora wa mbegu -Quality Declared Seeds (QDS), haziruhusiwi kutolewa nje ya wilaya zinapozalishiwa.

Kutoka katika Kijiji cha Ifiga, kata ya Ijombe wilayani Mbozi, Flora Mlowezi ni mmoja wa wataalamu wa mbegu, anayeiambia Nipashe anazalisha figiri, mchicha, mgagani, ngogwe na viungo mbalimbali na ameajiri watu wanne wanawake wawili na wanaume idadi kama hiyo.

"Tunapozalisha mbegu tunapunguza gharama za wakulima kuzinunua sokoni. Tuna uhakika kuwa zitaota na tutapata mazao tunayoyakusudia. Hakuna mbegu feki."

Anasifu utaalamu huo, lakini anataja changamoto hasa mtaji na pembejeo ili kuzalisha mbegu kwa mafanikio.

Flora anazungumzia ardhi kuwa ni tatizo akisema ni vigumu kuipata kwa sababu ni ya kukodi kwa gharama kubwa mfano, anasema mbegu huzalishwa wakati wa masika ambao kazi ya kilimo inafanyika na kwamba kukodisha shamba kunagharamu fedha nyingi. Anaeleza kuwa alipata eneo la kukodi la ukubwa wa mita 20 x 40 kwa Sh.200,000 ambayo ni gharama kubwa.

Anataja kukosekana mafunzo ya mara kwa mara kuwa ni changamoto, anakosa mwendelezo na kwamba kujifunza zaidi ni muhimu ili kuboresha utaalamu na ujuzi kulingana na wakati. Anagusia sheria za kukataza mbegu kuuzwa nje ya eneo la uzalishaji kuwa kikwazo na angependa ziruhusiwe kuuzwa sehemu mbalimbali.

Sheria inaagiza ziuzwe ndani ya eneo zilipozalishwa kwenye kata na wilaya akiomba ziruhusiwe kuuzwa sehemu nyingine ili kuongeza kipato. Anataja mahitaji ya pembejeo kama mbegu za kuzalisha mbegu (basic seeds), mbolea na viuatilifu vya asili na vya viwandani, kuwa ni muhimu kufanikisha kazi hiyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la MIICO, linalotoa mafunzo hayo, Catherine Mlaga, akizungumzia mradi wa kuzalisha mbegu za mboga za asili anasema unalenga kukabiliana na uhaba mkubwa wa chakula, udumavu na lishe duni kwenye ukanda unaozalisha vyakula wingi hasa mkoani Mbeya.

Anasema MIICO imejikita kwenye sekta ya kilimo ikijihusisha na kuhamasisha matumizi bora ya rasilimali za umma, kuleta usawa kijinsia, fursa za umiliki wa ardhi hasa vijana na wanawake na masuala ya uchumi ikiwamo kuzalisha vyakula vya kutosha kulisha familia.

"Tunaendeleza kilimo katika mikoa ya Iringa, Njombe, Songwe na Mbeya...Mbali na kilimo cha mboga na matunda tuko na kinamama wakulima wa mazao mengine kupaza sauti za wanawake walioko masokoni , shambani na maeneo yote ya kilimo ili zisikike na wawe sehemu ya uzalishaji, kuboresha maisha yao na familia zao na kuondokana na umaskini."

**MAKALA**

# Rushwa ya ngono ilivyo mwiba kwa mabinti wanahabari mafunzoni

**Na Mary Geofrey**



Waandishi wa habari wanawake na mdau kutoka kutoka benki ya PBZ, katika hafla ya kumkabidhi zawadi mwakilishi wa wanafunzi wa shule ya sekondari, mkoani Mtwara, mapema mwaka huu. **PICHA: MTANDAO.**

JITIHADA zinazofanywa na kinamama kufikia malengo yao, hata kuchangia ukuaji uchumi, bado zinakwamishwa na mfumo wa ubaguzi, unyanyasaji na ukatili wa kijinsia.

Hapo ndani yake kuna rushwa ya ngono, linalogeuzwa kuwa daraja au njia ya kutoa msaada, baadhi wakimfananisha mwanamama na kiumbe dhaifu, asiyemudu kuvuka viunzi katika jitihada zake.

Kutokana na hali hiyo, Nipashe inafanya utafiti kwa jamii hiyo, katika vyumba vya habari nchini.

Mwanafunzi wa Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma (SJMC) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Ummy Matinde, anasema wanakabiliwa na adha wanapoenda katika mafunzo kwa vitendo kwenye vyumba vya habari, wanaombwa rushwa ya ngono ili wasaidiwe.

Anasema wanaume waliopo kazini, wamekuwa wanawageuza vivutio na viburudisho, badala ya kuwachukulia ni wanafunzi kazini

"Ukifika tu unaanza kuitwa na kila mtu, unaombwa namba, unaombwa kukutana na bosi nje ya kazi kwa sababu amekusaidia kuingia katika ofisi hiyo kufanya (field)," anaeleza na kuendelea:

"Unapokataa kuwa na uhusiano na yoyote, unaanza kupewa vitisho. Kwa upande wa bosi yeye anakutisha kuwa, kazi ya uandishi wa habari ni kujituma, kuwa tayari kufanya kazi muda wowote na kuwa msikivu ili ufanikiwe."

Anaeleza yanayotisha ni kama kutoendelea na mafunzo katika ofisi hiyo na endapo hatabadilika watachukuliwa wanafunzi wengine wenye sifa na uwezo wa kujituma wakati wote.

Magdalena Jackson wa SJMC, anasema wanapoenda kuomba kufanya mafunzo kwa vitendo kwenye vyumba vya habari, hawapewi majibu ya moja kwa moja ama wamepata au la.

"Wahariri wanakuwa siyo wakweli, hawakwambii kuwa kama umekosa nafasi bali wanakuambia tutakuita endelea kusubiria lengo ni kuendelea kukuvuta karibu naye uzidi kuwasiliana naye na mwisho wa siku anaanza kukutongoza ili ukubali akusaidie kupata nafasi ya kufanya field," anasema Magdalena.

Anaeleza baadhi ya wahariri, huonyesha ishara ya mapenzi pasipo taarifa kamili na hata kuna wakati wanamfanyia visa mwanamke.

"Hivyo, kunatujengea woga wa kujifunza ukiwa unawaza labda unakosea au hujui kabisa na mwisho wa siku, mtu anaamua kuacha kuendelea kufanya field,"anasema Magdalena.

Mwanafunzi, Jojeth Adriano, anasema kutokuwapo nauli na chakula kwa wanafunzi wanaoenda kwenye vyumba vya habari, ni chanzo cha kuwaingiza mitegoni kwenye uhusiano.

"Unaenda field, unapangiwa kazi na majukumu anayopaswa kupewa mfanyakazi bila kujali tunajifunza, lakini hatupewi hata maji ya kunywa.

"Inabidi ujitegemee na mwisho wa siku wanaume waliopo kazini hutumia mwanya huo kutoa ofa ya chakula ili waturubuni. Unanunuliwa chakula siku ya kwanza, ya pili ya tatu..." anasimulia,.

Mwanafunzi mwingine, Abigaeli Silayo, anasema kuna wahariri na wafanyakazi wengine wanawapa majukumu yasiyosomea ikiwamo kupika chai, kuhudumia na kufanya usafi kwa sababu tu wamekataa kutembela nao.

"Unaanza kazi wiki ya kwanza, ya pili unaanza kutumwa kaniletee chai, kanifanyie hivi, mara unaanza kuambiwa upike chai na kuwapelekea, wakati niliomba 'field' ya kuandika habari au kutangaza," anasimulia.

Anasema hayo yanapokithiri, huwa wanatumia taarifa kwa walimu, ambao nao wanawasilisha kwa mamlaka za uongozi mahali hapo.

Jackline Ndalo, anasema:" Bado tunaamini tunaweza kuzivuka na kufikia malengo yetu ya kuwa wanahabari wabobezi ndani na nje ya mipaka ya nchi yetu," anasema Jackline.

Kwa upande wake, Mariam Magiri, kutoka Chuo Kikuu cha Tumaini tawi la Dar es Salaam (TUDARCO), anasema wanakwepa magumu hayo, wakivumilia kazi zaio kutotumika

**KINACHOJIRI MAGAZETINI**

Anasema magazetini kuna wahariri wanaowaweka baadhi ya mabinti vikwazo kazi zao zisitoke magazetini, pale hawakuhusiana kikazi.

"Ukiona hivyo, unaamua kukaa nyumbani kwa sababu unakuwa unamaliza nauli ukifika kazini huna unachokifanya. Unasubiri siku ya mwalimu kuja kazini kwako ndio unaenda ili akukute," anasema Mariam,

Anaeleza zaidi wahariri wanapokataliwa na wanafunzi wa mafunzo kazini, wanachofanya pia ni kutishia kuwachafulia katika ripoti zao, ili kuyafanya vizuri wakubaliwe na uhusiano.

Mariam anasema kinachowakatisha tamaa ya kuendelea na kazi ya uandishi wa habari, siyo unyanyasaji kingono, bali ni mazingira magumu ya kufanyia kazi.

Anasema, pia wanahabari wana maslahi duni kuishi katika mazingira magumu, wanahabari wanawake huwaajiriwi na kutoshirikishwa ngazi za kuamua

**KUTOKALHRC**

Utafiti wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) mwaka 2018 ulionyesha rushwa ya ngono makazini na vyuoni bado ni shida changamoto kubwa ikiwamo upande wa wanahabari wa kike.

Ripoti hiyo, ilibainisha wanaokumbana na ugumu kwa wanawake ambao wanaoenda kutafuta kazi, mabinti wanaombwa sana rushwa ya ngono ili waweze kupewa kazi au hata kupandishwa kwenye na kufahamika, tatizo kubwa kinamama kwenye habari.

Mwezi Oktoba mwaka juzi, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ilitafiti rushwa ya ngono katika baadhi ya vyuo vikuu nchini vikiwamo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) na kubaini rushwa, hasa ikijikuta katika kigezo cha mwanama kudaiwa afaulu mtihani.

Sheria ya Kupambana na kuzuwia Rushwa nchini, imeweka kifungu mahsusi kwa mwenye mamlaka kudai au kuomba rushwa ya ngono, ikiwamo kuajiri, kupandisha cheo au kutolewa haki na katika yaliofanywa hivi karibuni, ni moja ya makosa saba ya uhujumu uchumi.

**KUTOKA WILDAF**

Mkurugenzi wa Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika (WiLDAF) Anna Kulaya, anasema sehemu ya kazi inapaswa kuwa salama kwa mfanyakazi kwa sababu ni sehemu ambayo mfanyakazi anachukua muda mrefu kuishi.

Anasema mwaka 2018 walitafiti sehemu za kazi na wafanyakazi, walianika kuwapo rushwa ya ngono hasa kwa wanawake.

Katika kukabiliana na unyanyasaji kingono pamoja na rushwa hiyo, serikali iliandaa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA 2017/18 - 2021/22).

Ni mwongozo unaelekeza namna ya kuunda kamati, mgawanyo wa majukumu na utendaji wa kamati za ulinzi wa wanawake na watoto kuanzia ngazi ya Taifa, Tawala za Mikoa hadi Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuweka utaratibu na uwiano wa utekelezaji wa mpango kazi.

Malengo makuu ya mpango huo ni kuelekeza taratibu za kuanzisha kamati katika ngazi zote pamoja na majukumu yake, kuweka utaratibu wa utoaji wa taarifa sahihi za utekelezaji, kuelekeza muda na taratibu za uendeshaji wa vikao vya kamati na kuweka vigezo vya uwakilishi kwa wajumbe wa Kamati.

**Nini kifanyike?**

Mshauri Mwandamizi wa Afya ya Jamii na Jinsia, Wizara ya Afya, Dk. Katanta Simwanza, anasema kundi la watu walioko vyuoni hawana pa kuzungumzia adha za rushwa ya ngono zinazowakabili, na hivyo kuna haja ya kuunda madawati ya jinsia vyuoni ili kuwapa jukwaa la kuelezea masaibu yao.

**Makala hii ni kwa mujibu utafiti uliofanywa na mwandishi.**

# Jacob Zuma kutumikia kifungo nyumbani

**Johannesburg,** AFRIKA KUSINI

RAIS wa zamani wa Afrika Kusini, Jacob Zuma, amerejea nyumbani baada ya kutolewa hospitali, ripoti ya chombo vya habari kimoja kimesema sasa anatarajiwa kutumikia kifungo chake chote kwa kuidharau mahakama.

Usiku wa kwanza baada ya kutoka Hospitali , alilala nyumbani kwake Nkandla huko KwaZulu-Natal baada ya kutoka hospitali mjini Gauteng, tovuti ya Times Live iliripoti.

Inasemekana kurejea kwake kunafanywa kimya kimya.

Wakfu wa Zuma wiki iliyopita ulisema kuwa hautatoa maelezo kuhusu ni lini atatolewa hospitali kutokana na sababu za usalama.

Zuma alilazwa katika hospitali ya kijeshi mwezi uliopita nje ya gereza kutokana na ugonjwa mabao haukutajwa na kufanyiwa upasuaji.

Alijisalimisha mwenyewe gerezani mwezi Julai baada ya kuhukumiwa kifungo cha miezi 15 kwa kupuuza agizo la kufika mbele ya jopo la mahakama la kiuchunguzi wa ufisadi wakati wa utawala wake.

Alipewa msamaha wa matibabu mapema mwezi huu. Sasa anatarajiwa kutumikia muda wake wote wa gerezani nyumbani baada ya kutolewa hospitalini.

**BBC**



Mwanaume akisukuma pikipiki ndani ya maji baada ya jiji la Karachi nchini Pakistani kukumbwa na mafuriko kutokana na mvua nyingi kuendelea kunyesha hadi jana (**PICHA: AFP**)

# Fedha umma Dola milioni 73 zatumika vibaya Sudan Kusini

**Geneva,** USWISI

ZAIDI ya dola milioni 73 za rasilimali za umma zimetumiwa vibaya na viongozi wa Sudan Kusini tangu mwaka 2018, imebaini ripoti ya Tume ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa iliyotolewa wiki hii huko Geneva.

Uporaji huo mkubwa wa rasilimali za serikali unatishia mchakato wa amani, ambao uko hatarini katika nchi changa, Umoja wa Mataifa umeonya.

Kwa upande wa waandishi wa ripoti hii walisema kiwango cha ubadhirifu wa fedha za umma, Sudan Kusini kinatisha.

Tume ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa iliripoti kutopotea kwa dola milioni 73 tangu mwaka 2018, pamoja na karibu dola milioni 39 katika kipindi cha chini ya miezi miwili. "Na bado, kiasi hiki kinaonesha tu sehemu ya jumla ya pesa zilizoporwa", imeonya Tume ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa.

Uporaji wa mali ya umma unawanyima Wasudan Kusini huduma za kimsingi.

Umoja wa Mataifa unashutumu viongozi wa Sudan Kusini kuanzisha mfumo usio rasmi kwa makusudi wa kukusanya mapato ya mafuta, kwa rasilimali kuu ya nchi hiyo.

Mfumo ambao ulifanya kazi bila uwazi wowote au udhibiti huru.

Ripoti hiyo inahusisha wanasiasa, maofisa wa serikali, wanajeshi, lakini pia benki za kimataifa, ambazo sehemu nyingne ya pesa imepita.

Kwa upande wa Umoja wa Mataifa (UN), ulisema, mabadiliko hayo yanawanyima Wasudan Kusini huduma za kimsingi, katika nchi ambayo asilimia 80 ya raia wake wanaishi katika umasikini uliokithiri.

**RFI**

## Mwanahabari atuhumiwa kwa ugaidi

**Kinshasa,** DRC

MWANDISHI wa habari kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo ( DRC), Sosthène Kambidi, ambaye anaripoti AFP, Actualité.cd na RFI, aliyefunguliwa mashtaka ya kuwa na taarifa kuhusu mauaji ya watalaam wawili wa Umoja wa Mataifa (UN), Michael Sharp na Zaida Catalan, mwaka 2017 katika jimbo la Kasai, anaendelea kuzuiwa.

Kambidi alikamatwa siku ya Jumanne wiki hii, usiku jijini Kinshasa sasa sio shahidi katika kesi hiyo bali ni mshukiwa, kwa mujibu wa viongozi wa mashtaka.

Kesi yake inatarajia kuanza ndani ya siku mbili au tatu katika mahakama ya kijeshi.

Sosthène Kambidi alikuwa akitoa kila siku ripoti kuhusu mauaji ya raia katika majimbo ya Kasai na alishiriki katika uchunguzi wa mauaji ya wataalam wawili wa Umoja wa Mataifa, Michael Sharp na Zaida Catalan.

Mamlaka inataka kujua habari zake zinatoka wapi.

Sosthène Kambidi alihojiwa kwa mara ya kwanza siku ya Jumatano na aliweza kupata wakili wa kumsaidia katika utetezi wake, Maître Kabongo.

Kulingana vyanzo vya kuaminika, upande wa mashtaka unataka kujua chanzo cha habari yake kuhusu mauaji ya wataalam wawili wa UN, yaliyotokea mwaka 2017 huko Kasai na kujua jinsi video ya mauaji ya wataalamu hao ilipatikana.

Kwa upande wake, Thomas Fessy, mwakilishi wa shirika lisilo la kiserikali la haki za binadamu la Human Rights Watch kwa DRC, ana wasiwasi juu ya hali ya kukamatwa huko na habari inayoonyesha mashtaka. **RFI**

## Nigeria yawakamata washukiwa wa utekaji nyara wanafunzi

**Lagos,** NIGERIA

WATU watatu wanaoshukiwa kuhusika na utekaji nyara wa zaidi ya wanafunzi 100 wa shule katika jimbo la Kaduna nchini Nigeria wamekamatwa, polisi wanasema.

Watu hao ni miongoni mwa washukiwa 50 wanaoaminiwa kuwa wanachama wa magange tofauti yanayowahangaisha wanavijiji katika maeneo ya kaskazini -magharibi na kati mwa Nigeria.

Msemaji wa Polisi Frank Mba anasema vikosi vya usalama vinawafuatilia watu wengine 22 ambao ni wanachama wa genge ambalo ni sehemu ya utekaji nyara huo.

Hayo yanajiri wakati mamlaka za majimbo katika maeneo hayo yakiwatumia makundi ya walinzi kusaidia kudhibiti usalama.

Julai 5, watu wenye silaha walivamia shule ya upili ya Bethel Baptist huko Kaduna na kuwateka nyara zaidi ya wanafunzi 121.

Baadhi ya waathiriwa wameachiliwa, kwa mafungu huku wanafunzi 10 wakiachiwa siku chache zilizopita. Wanafunzi 20 bado wanashikiliwa mateka.

Wazazi wa watoto waliotekwa nyara wameripotiwa kulipa kiasi kikubwa cha pesa kama fidia, ili watoto wao waachiliwe lakini madai hayo hayajathibitishwa rasmi.

Utekaji nyara wa wanafunzi hao ulikuwa wa nne katika shule za Kaduna katika miezi michache iliyopita.

Utekaji nyara kama huo umefanyika katika majimbo jirani ya Zamfara, Niger na Katsina, ambayo yameshuhudia ukosefu mbaya wa usalama.

**BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MATANGAZO MCHANGANYIKO**

PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA ENTEPRISES FINANCE LIMITED (EFL). KWA MAWASILIANO ZAIDI **TUPIGIE:0677 111 333 AU 0758 112 332**

**MATANGAZO MCHANGANYIKO**

KIWANJA KINAUZWA

KIWANJA KIPO KISUKURU JKT UKUBWA SQM 2252 KINA HATI, BEI MILIONI 60. **MAWASILIANO 0786 857523 Au 0655 857523.**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676**

## KUPOTEA KWA VYETI



**HAROUB SHARIFF KHAMIS** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne Chenye index namba **S0381/0024** Kilichotolewa na **UTAANI SEKONDARI** mwaka **1990.** Cheti cha kidato cha sita Chenye index namba **S0309/0026** kilichotolewa na **FIDEL CASTRO SEKONDARI** mwaka **1993.** Yeyote atakayeviona atoe taarifa Polisi. Taarifa ya Polisi **DAR/MAG/RB/463239/2021.**

116476002

## KUPOTEA KWA CHETI



**DONALD JOHN** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0333/0091** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MWANZA SEKONDARI mwaka 2018.**
Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.Taarifa ya polisi: **KISH/RB/252/2021.**

116476702

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**SARENI NADA IRAQA** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YAKE YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 187 CXU.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **KRT/RB/6943/2021.**

116476102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA
MAHALI DODOMA
MAOMBI MADOGO NA. 165 YA 2021
BAINA YA
MATHIAS ZAKARIA……………………………MRUFANI
DHIDI YA
HAMIS ALLY……………………………. MRUFANIWA
KWA:
HAMIS ALLY
YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria **tarehe 30.09.2021 saa 3:00 asubuhi.** Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.

**ANGALIZO: -** kama hukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likidhibitisha kuwa umepokea Hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri /Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 21 ya mwezi wa september,2021.

MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ,
DODOMA.

116476502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
KATIKA MAHAKAMA
YA WILAYA YA BUKOBA
HATI YA KUITWA SHAURINI(SUMMONS)
Shauri la rufaa Mahakama
ya Wilaya ya Bukoba**

**JEREMIA TIIBO-Appellant
Dhidi ya
Abela Alexander Msikula-Respondent
Kwa Abela Alexander Msikula
K.K Afisa Mtendaji Kata Katoma**

Elewa kuwa kesi ya rufaa hiyo hapo juiu itatajwa/itasikilizwa/kusomewa hukumu **tarehe 12.10.2021** asubuhi katika mahakama ya Wilaya hivyo unapaswa kuhudhuria bila kukosa.
Imerolewa kwa mkono wangu na mhuri wa mahakama hii leo **tarehe 17/9/2021**

**HAKIMU MKAZI MFAWIDHI
MAHAKAMA YA WILAYA BUKOBA**

116476702

## TANGAZO KUPOTEA OFA YA KIWANJA

**Athuman Juma Mangilo** ambaye ni msimamizi wa mirathi ya Marehemu **Asha Fundi** anatangaza kupotelewa na Ofa ya kiwanja namba **43, Kitalu 'I' Kambarage** Manispaa ya Shinyanga. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi Kilichopo karibu. Control namba: **9910830352550.**

116476902

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA
YA WILAYA YA MBOZI MKOA
SONGWE
SHAURI NO.162021
DOROTHEA JONAS MARIJANI::::::::::::::::::::::::MDAI
DHIDI YA
1.KANYENYE MABULA:::::::::::::::::::::::::::::::::;MDAIWA
2.SAMUEL JEREMIAH:::::::::::::::::::::::::::::::::MDAIWA
3.EMMANUEL KAMAKA:::::::::::::::::::::::::::::::MDAIWA**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

KWA:
**SAMUEL JEREMIAH,**
Fahamu kwamba DOROTHEA JONAS MARIJANI amefungua shauri dhidi yako katika baraza hili.
Shauri limepangwa kutajwa tarehe 01/10/2021 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mh.T.Munzerere Mwenyekiti wa Baraza.Unatakiwa kuleta utetezi wako wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya wito huu.
Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Mbozi-Songwe.
Unaamriwakuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria.Ofisi za baraza zipo karibu na eneo la mnadani Vwawa.
Kumbuka:Usipo hudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na lakiri/muhuri wa baraza hili leo **tarehe 17/09/2021.**

**T.Munzerere
MWENYEKITI
17/09/2021.**

116477402

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**BENJAMINI LEE VIOLA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T.468 AAB** AINA YA LANDCRUISER RANGI YA LIGHTGOLD/CRAY. CHASSIS NAMBA **HDJ810029075.** ENGINE NAMBA 1HD0056567.YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI MBE/MBE/RB/463702/2021

116477502

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA
LAND DIVISION AT BUKOBA
LAND APPEAL NO 11 OF 2021**

From the decision of the District Land and Housing Tribunal of Bukoba District in Land Appl No 127/of 2020 and Original Ward Tribunal of Ward application No……of 20…..

**Nelson Saulo…………………..APPELLANT
VERSUS
Solomon Saul & Another**

**To: Solomon Saul
c/o WEO Mugajwale
Bukoba District-0747206918**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for hearing on the 04 day of Octoba,2021 at 9.00 a.m before Hon Mwaipopo Judge.

**YOU ARE** required to appear in this court on the fixed date without fail.

Copy of the petition of appeal is attached here to and you may file your reply thereto into two days prior to the fixed date of hearing and serve a copy to the appellant. Given under my hand and seal of the court this 13,day of Sept,2021

REGISRAR

116476802

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
FOR DODOMA
AT DODOMA
PROBATE AND ADMINISTRATION
CAUSE NO.117 OF 2021**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE
LAWRENCE JOHN MATEE
AND
IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS
OF ADMINISTRATION BY
MWAJUMA LAWRENCE MATEE**

**GENERAL CITATION
(RULE 75 OF PROBATE RULES GN.369 OF 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 29 day of 09 2021.

**Dated at Dodoma this 14 day of September 2021.**

RESIDENT MAGISTRATE

116476902

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

116460202

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

TOM alipooa alidhani kuwa ataishi kwa amani, furaha na kupata utulivu kama inavyokuwa kwa rafiki na wenzake wote waliofanya hivyo.
Siku zote ndoa ni masikilizano, maelewano, na anayeoa hupata furaha na heshima. Kinyume chake, kwake amekuwa ni misukosuko, mikosi na balaa. Badala ya kuwa ndoa yenye furaha, akajiingiza kwenye mtego hatari ambao hata baada ya kuufahamu, hakuweza kuutegua tena. Alichelewa. Ukawa ni mwanzo ni vilio, maafa na mtiririko wa mambo ya kushangaza.
Hebu pata kila nakala ya gazeti hili kufuatilia kisa hiki cha kushangaza na kusikitisha.

# Namsaka Mke Wangu-12

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

"Nenda basi kaoge, na mimi niende tuje kulala." alisema.

Lilikuwa ni kosa kubwa kwa Sam. Ni kosa la kiufundi. Alipoingia bafuni. Haraka, Tedi alikwenda alifungua mkoba wake na kutoa kidonge alichopewa na Tom. Akakitumbukiza kwenye glasi ya bia ilikuwa nusu. Alichofanya akaongeza bila nyingine na kujaza.

Aliporejea, Sam alivua nguo na kubaki na bukta. Bila kuuliza akanyanyua glasi ile ile na kuimimina kinywani.

Nusu dakika baadaye alianza kuona dabo dabo. Nusu nyingine aliyobaki akalala fofofo. Akaanza na kukoroma akitoa povu ambalo lilianza kumtisha hata muwekaji mwenyewe.

Hata hivyo alikumbuka maneno aliyoambiwa na Tom kuwa hatokufa, ila atalala usingizi kwa masaa kadhaa, halafu ataamka.

Kazi iliyofuata ambayo kwake ndiyo aliiona ni kubwa zaidi ni kutafuta vitu ambavyo vilihitajika.

Kwa bahati nzuri alijua nini kilihitaji kutafutwa na nini kuachwa. Tatizo ni muda wa kutafuta na mada gani vielelezo vitapatikana.

Ilimchukua nusu saa kusaka huku na huko. Lakini ni vielelezo vitatu tu ambavyo aliona huenda vinaweza kumsaidia Tom. Baada kuangaza huku na huko, akafanikiwa tena kupata vitu viwili ambavyo vinavyofanana na anavyohitaji aliyemwagiza. Mwisho kabisa akaifuata simu ya mkononi. Akachukua na kuweka kwenye mkoba wake.

Kazi ikawa imekwisha. Alitumia saa moja na dakika 40, tangu alipoingia kwenye nyumba ya Sam na kukamilisha kazi ile. Aliondoka kwa tahadhari ili asishtukiwe na mtu yoyote. Ilikuwa ni saa sita na dakika ishirini usiku.


Alipotoka alitembea hatua kadhaa. Akasimamisha bodaboda na kuelekea anakoishi na mpenzi wake Tom.

************************

Wakati huo, Tom alikuwa amekusanya kila kitu. Hakutaka tena kukaa pale. Hii si kwa ajili ya usalama wake, bali ni kwa ajili ya Tedi.

Alijua kwa vyovyote Sam atakapozinduka, basi atamtafuta kila mahali Tedi sehemu yoyote ile. Hata ikiwezekana kuipindua Morogoro yote kichwa chini miguu juu.

Alisikia sauti ya bodaboda ikisimama karibu na geti la nyumba ile ya kulala wageni. Dakika moja baadaye Tedi aliingia.




**"Walitoka ndani na mabegi yao. Walisimamisha bodaboda. Wakapanda wote wawili. Kituo cha kwanza kikawa ni Mikese. Wakatafuta nyumba moja nzuri ya kulala wageni. Hawakutaka hoteli, wala nyumba ya wageni iliyochanganyikana na baa. Hii ni kwa ajili ya utulivu na usalama wao.**

Alionekana mchovu, mwenye mawazo mengi, lakini mwenye tabasamu. "Tayari." Alimwambia Tom.

"Tayari nini?"

"Kila kitu. Vyote ulivyoniambia nimekamilisha." Alijibu kwa uhakika wa kile anachokisema.

"Hajafanya matata yoyote?" Tom aliuliza. Lakini lilikuwa ni swali ya mtego ambalo Tedi alijua maana yake.

"Mhh mwanaume wewe, wivu tu unakusumbua. Hajanifanya kitu chochote. We, nilikuwa makini kama nalinda benki."

"Sasa kama kila kitu tayari, hapa tuondoke. Sam ni mtu maarufu hapa Morogoro. Atakapoamka, mtu wa kwanza kumsaka ni wewe. Na hutaki tena kurejea Morogoro, unalifahamu hilo?"

"Nalifahamu. Ila nimefanya hivyo kwa sababu yako. Nimetokea tu kukumini, lakini kama unanitupa, basi mimi nitarudi kwetu Singida."

Tom aliitazama saa yake kwenye simu, ikamwambia ni saa saba na robo usiku.

"Tunaondoka muda huu."

"Tunakwenda wapi?"

"Popote pale, lakini ni sehemu ya usalama zaidi."

Tedi si tu kwamba alikuwa ameshamzoea Tom, lakini alitokea kumuamini. Hakuna chochote alichomwambia au kumfanyia kikaleta matokeo hasi.

"Ndiyo maana alimkubalia chochote alichomwambia."

"Walitoka ndani na mabegi yao. Walisimamisha bodaboda. Wakapanda wote wawili. Kituo cha kwanza kikawa ni Mikese.Wakatafuta nyumba moja nzuri ya kulala wageni. Hawakutaka hoteli, wala nyumba ya wageni iliyochanganyikana na baa. Hii ni kwa ajili ya utulivu na usalama wao.

*********************************

Ilikuwa ni saa tano asubuhi. Baada ya kulala, kuamka, kwenda kuoga na kupata kifungua kinywa ambacho kilikuwa ni chapati, mayai ya kukaanga na chai, walijifungua chumbani na kuanza kukagua vilivyodhaniwa kuwa ni vielelezo ambavyo Tom alimtuma Tedi kwenda kuvifuata kwa Sam.

Kwanza walipitia barua kadhaa ambazo kwao hazikuwa na maana yoyote.

Baadaye walikutana na albamu za picha za mnato. Macho yao walitua kwenye picha moja ambayo iliwafanya washtuke.

Waliishangaa kwa dakika moja nzima. "Nadhani hii ni picha ya miaka kama kumi iliyopita." Tedi alimshtua Tom ambaye alionekana kuwa kimya na mshangao zaidi kuliko mwenzake.

Wala haukuhitaji ufundi au utaalam wowote kujua ni picha ya zamani. Hata watu waliokuwa kwenye picha hiyo, walionekana bado ni vijana sana kuliko sasa, na nguo zao, viatu vyote vilikuwa vya mitindo ya kizamani.

Ilikuwa ni picha ya Sam na Farida. Kwa jinsi walivyopiga ilionekana kuwa ni wapenzi.

"Kumbe mke wangu alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na Sam miaka ya nyuma kabla sijamuoa." Alijiambia mwenyewe kimya kimya.

Pamoja na mshangao huo, lakini bado alionekana kuwa na kiu ya kutaka kujua mengi. Kuwa na mke ambaye zamani alikuwa na mpenzi ni kitu cha kawaida. Alichoshangaa tu ni kuwa alikuwa ni mapenzi wa Sam.

"Sasa kwa nini baada ya kuolewa, alinikimbia siku saba tu baada ya ndoa, akarudi kwa Sam?" Hilo ndilo likaanza kumuumiza kichwa.

Vielelezo karibuni vyote walivyovipitofautiana sana. Vilionyesha tu kuwa Sam na Farida walikuwa ni wapenzi. Zilikuwa ni picha ambazo zilionyesha wapo sehemu mbalimbali. Na zingine Tom alishindwa kuziangalia vizuri kutokana na jinsi walivyokaa na kupiga kimahaba zaidi.

"Kilichobaki sasa ni simu tu." Tedi alimkabidhi simu.

"Iwashe." Tom alimwambia.

"Ina 'pasiwedi.' Alilalamika Tedi.

"Ilete hapa mimi ndiye mtaalam wa hivyo vitu."

Zilichikua dakika tano hivi, Tom kuivunja 'pasiwedi' na simu ilichokuliwa kutoka kwa Sam ikafunguka. Sehemu ambazo walizitaji zaidi ni kwenye picha na meseji.

Walianza kuziangalia picha. Nyingi hazikutofautiana na zile za kwanza. Pamoja na hayo kwenye simu kulikuwa na picha zilizoonekana zimepigwa kwenye miaka ya karibuni, miaka miwili au mmoja, kabla ya kuolewa. Siku ilionyesha mpaka tarehe zilizopigwa.

Baada ya kuridhika na kila kitu walichokiona, waliingia kwenye meseji. Baada ya kukutana na meseji nyingi zingine za kufurahisha, kuchekesha na kusikitisha, walikutana na zile ambazo walizihitaji.

Yalikuwa ni majibizano ya Sam na Farida.

"Mwaka wa kumi sasa unasema utanioa, lakini mpaka sasa naona kimya."

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# TANZANITE DIMBANI ERITREA, TWIGA STARS YAENDA SAUZI

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI kikosi cha Timu ya Soka ya Taifa ya vijana umri chini ya miaka 20 (Tanzanite Queens), kinatarajia kuwakabili yosso wenzao wa Eritrea katika mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia itakayochezwa leo jijini Asmara nchini humo.

Timu hizo zinatarajiwa kurudiana Oktoba 9, mwaka huu hapa jijini Dar es Salaam, wakati fainali za mashindano hayo zitachezwa nchini Costa Rica.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Edna Lema, alisema wachezaji wake wamejiandaa vyema kuelekea mchezo huo na wanaamini watapata matokeo chanya.

Edna alisema wanatarajia kuanza vyema kampeni ya kuelekea katika fainali hizo na wamewataka wachezaji kuongeza umakini watakapokuwa na mpira.

Kocha huyo alisema wachezaji wao wameimarika na wamewajenga kuhakikisha wanaanza vizuri kampeni hiyo huku ndoto yao ni kuweka rekodi ya kufuzu mashindano hayo kwa mara ya kwanza.

"Tunajua mechi zote ni ngumu, sisi tumekuja huku kupambana kuhakikisha tunashinda na kurahisisha mchezo wa marudiano, tutahakikisha tunaanza vyema michuano hii," alisema kiungo huyo wa zamani wa Twiga Stars.

Afrika itatoa timu mbili kwenda kwenye fainali hizo, nafasi ambazo ndizo zinashindaniwa kwenye michuano hiyo ya mtoano.

Ratiba inaonyesha kuwa mshindi kati ya Tanzanite Queens dhidi Eritrea atakutana na Burundi au Namibia.

Wakati huo huo, Ofisa Habari wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo, amesema kikosi cha Twiga Stars kinatarajia kuondoka nchini kesho alfajiri kuelekea Afrika Kusini kwa ajili ya kushiriki mashindano ya COSAFA.

Ndimbo alisema maandalizi ya kuelekea safari hiyo yamekamilika na wakiwa huko wataanza kuwania kombe la michuano hiyo



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makala, akizungumza kuhusu maandalizi ya mechi kati ya viongozi wa dini na mabalozi wanaowakilisha mataifa yao hapa nchini utakaochezwa leo mchana kabla ya mchezo wa Ngao ya Jamii kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE**

# TFF kupambana na Covid 19

**Na Saada Akida**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF), limeingia makubaliano na Wizara ya Afya kwa ajili ya kuunga mkono juhudi za serikali katika vita dhidi ya mapambano ya ugonjwa wa uviko 19.

TFF kwa kushurikiana na wizara hiyo imeweka mahema kwa ajili ya upatikanaji wa huduma ya chanjo nje na ndani ya Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Lakini pia TFF imetoa tiketi 100 na zawadi kama motisha kwa idadi hiyo ya mashabiki watakaokuwa wa kwanza wakupata chanjo ya COVID 19.

Katibu Mkuu wa TFF, Wilfred Kidao, alisema wameamua kuunga juhudi za serikali za ili kupambana na ugonjwa huo ambao umesababisha mashabiki kutoingia uwanjani.

Kidao alisema wameanza kampeni hiyo katika mchezo wa Ngao ya Jamii utakaochezwa leo kwa kuwakutanisha Simba na Yanga na baadaye wataendelea kuhamasisha katika michezo mingine inayofuata ikiwamo ya kimataifa.

Naye Mwakilishi wa Wizara ya Afya ambaye pia ni Mratibu wa Afya Dar es Salaam, Agnes Mgaya, alisema wanaishukuru TFF kwa jitihada walizozionyesha katika kupambana na ugonjwa huu ambao umekuwa tishio.

## Mbeya City yaota mashindano CAF

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Mbeya City, Mathias Lule, ameweka wazi hafikirii kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu lakini akafunguka malengo yake ni kumaliza kwenye nafasi nne za juu na kufuzu kushiriki mashindano ya kimataifa hapo mwakani.

Akizungumza na gazeti hili jana, Lule alisema msimu uliopita haukuwa mzuri kwake lakini ana matarajio ya kufanya vyema na kufikia malengo kwenye msimu unaokuja.

Lule alisema anakiamini kikosi chake baada ya kufanyia kazi upungufu uliowagharimu katika msimu uliomalizika ikiwamo kusajili wachezaji wapya wa ndani na nje ya Tanzania.

"Ligi ya msimu huu itakuwa ngumu na yenye ushindani, timu nyingi zimeboresha vikosi na mabenchi yao ya ufundi, tumejiandaa vizuri kupambana kufikia malengo yetu ya kumaliza katika nafasi za juu ila sio ubingwa," alisema Lule.

Aliongeza kila mechi kwao itakuwa kama fainali kwa sababu wanahitaji kutimiza ndoto zao kushiriki mashindano ya kimataifa kwa mara ya pili.

Mbeya City itafungua dimba la Ligi Kuu Tanzania Bara kwa kuwakaribisha 'Maafande' wa Prisons hapo Septemba 28, mwaka huu kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya.

## Polisi Tanzania yaipania KMC FC

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Polisi Tanzania yenye maskani yake mjini Moshi, Malale Hamsini, amesema amejipanga kuondoka na pointi tatu muhimu katika mchezo wake wa kwanza dhidi ya KMC FC utakaochezwa Jumatano kwenye Uwanja wa Ushirika Septemba 29, mwaka huu mkoani Kilimanjaro.

Akizungumza na gazeti hili jana, Malale alisema wamejipanga vizuri kuhakikisha wanaanza msimu kwa kupata matokeo chanya na kujiongezea morali kuelekea mchezo unaofuata. Malale alisema anakifahamu kikosi cha KMC, hivyo amejiandaa kukabiliana na ushindani.

"Tunaendelea vyema na mazoezi kuelekea mechi yetu ya ufunguzi, tunawaomba mashabiki wetu watupe ushirikiano kama walivyotuonyesha katika msimu uliopita tumewaandalia matokeo bora zaidi," alisema Malale.

Aliongeza maandalizi ya muda mrefu waliyofanya pamoja na mechi za kirafiki walizocheza zimewasaidia kuwaweka tayari wachezaji wake.

"Tunahitaji kumaliza kwenye 'Nne Bora', hivyo hatutabweteka, kila mechi kwetu ni muhimu, tunahitaji kushinda iwe nyumbani au ugenini, tunawakumbusha mashabiki wetu pia kuendelea kutuunga mkono," Malale aliongeza.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### NDOMBELE NA MARTIAL

KLABU ya Tottenham Hotspur inaweza kuwa tayari kumwachilia kiungo wake raia wa Ufaransa, Tanguy Ndombele mwenye umri wa miaka 24, katika makubaliano ya kubadilishana na raia mwenzake mshambuliaji wa Manchester United, Anthony Martial. (**Express**)

### LIVERPOOL YAMTAKA BOWEN

LIVERPOOL bado inaweza kuwasilisha ombi la kumsajili mshambuliaji wa England na West Ham, Jarrod Bowen. Walihusishwa na ofa ya pauni milioni 20 kwenye dirisha la majira ya joto. **(Liverpool Echo)**

### CHIESA ATAJWA DORTMUND

BORUSSIA Dortmund inaweza kuwasilisha ombi la kumsajili winga wa Juventus na Italia, Federico Chiesa mwenye umri wa miaka 23, endapo klabu hiyo ya Bundesliga itampoteza mshambuliaji wa Norway, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 21, msimu ujao wa joto. **(Calciomercato)**

### HAALAND KWENYE RADA

LIVERPOOL nayo imejiunga kwenye mbio za kutaka kumsajili Erling Haaland wakati Mkurugenzi Mtendaji wa Borussia Dortmund, Hans-Joachim Watzke akikiri itakuwa vigumu kwa nyota huyo kubakia hapo msimu ujao wa joto. **(Mundo Deportivo, via Mail)**

### ANSENSIO SOKONI

KIUNGO wa kati wa Real Madrid, Marco Asensio mwenye umri wa miaka 25, ni miongoni mwa wachezaji wanaolengwa na Liverpool. **(Fichajes. Net, via Sun)**

### FONSECA ALIIKOSA SPURS

KOCHA Paulo Fonseca raia wa Ureno mwenye asili ya Msumbiji (48), amesema hatua yake ya kuinoa Tottenham Hotspur ilitibuka kwa sababu Mkurugenzi wa Michezo, Fabio Paratici alitaka Spurs icheze mpira wa "kujilinda"**. (Telegraph)**

### BAYERN YAJIPANGA

KOCHA wa Bayern Munich, Julian Nagelsmann amesema bado hajazungumza na Mkurugenzi wa Michezo, Hasan Salihamidzic kumhusu Antonio Rudiger, ambaye mkataba wake unamalizika mwisho wa msimu huu kule Chelsea**.(Eurosport)**

### ARSENAL MAMBO MAGUMU

ARSENAL inatarajia kumpoteza mshambuliaji Mfaransa, Alexandre Lacazette bure wakati mkataba wake utamalizika msimu wa joto, na Atletico Madrid inavutiwa na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30. **(Le10 Sport, via Mirror)**

### LACAZETTE AGOMBEWA

KLABU ya Hispania, Ujerumani na Italia zinavutiwa na Alexandre Lacazette, wakati West Ham na Crystal Palace zinaweza kumpa nafasi ya kubaki kwenye Ligi Kuu England. **(90min)**

### DEMBELE ANUKIA UNITED

MANCHESTER United wamefanya mawasiliano na Barcelona juu ya uhamisho wa mshambuliaji wa Ufaransa, Ousmane Dembele mwenye umri wa miaka 24.. **(El Nacional, via MEN)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# BAYERN YAMWEKEA MIPANGO RUDIGER

**Ni baada ya beki huyo kuonyesha dalili za kutaka kuondoka London huku...**

MUNICH, Ujerumani

MABOSI wa Bayern Munich wamejiunga na Paris Saint-Germain pamoja na Real Madrid kumwania beki wa Chelsea, Antonio Rudiger, ambaye mkataba wake unaelekea ukingoni katika klabu yake inayotumia Uwanja wa Stamford Bridge, kwa mujibu wa Bild.

Bayern Munich wanafuatilia hali ya Rudiger ambaye hadi sasa hajaongeza mkataba na Chelsea na mkataba wake wa sasa unakamilika msimu ujao wa kipindi cha majira ya joto.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, Bayern Munich imekuwa ikiwasiliana na wakala wa Rudiger na kaka yake, Sahr Senesie, lakini mazungumzo hayo ni ya awali kwa sasa.

Upande wa kocha, Julian Nagelsmann unamchukulia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 kama mbadala mzuri wa Niklas Sule endapo ataondoka pale Allianz Arena msimu ujao wa joto.

Kama ilivyo kwa Rudiger, mkataba wa Sule unamalizika mwishoni mwa msimu huu, na amezuia mazungumzo na bado hajaamua ikiwa anataka kuendelea na mabingwa hao wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga.

Mazungumzo yanaendelea kati ya Chelsea na Rudiger kuhusu kuongeza mkataba, ingawa Blues hao wanabaki kuwa waangalifu juu ya madai yake.

Mchezaji mwenyewe anafurahi kukaa London, lakini anajua kutokana na umri wake, mkataba wake unaofuata unaweza kuwa wa mwisho wa fedha nyingi.

MECHI KALI
HOME
SIMBA
1.50 | 3.20 | 3.30
YOUNG AFRICANS
AWAY
1 WEKA PESA.
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4 - WEKA PESA.
- FUNGUA MENYU YA HALOPESA
- CHAGUA LIPA/LIPIA BILI
- WEKA NAMBA YA KAMPUNI 150888, KUMBUKUMBU 888.
- KISHA WEKA 500 AU ZAIDI.
SEND
2 WEKA BET.
- PIGA *150*87#
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 517,3

# JACKPOT SPORTPESA YAFIKA NUSU BILIONI




**Na Mwandishi Wetu**

SPORTPESA wamerudi kivingine huku Jackpot yao ikifikia nusu bilioni ambapo huenda ikapata mshindi wiki za hivi karibuni ukizingatia mshindi aliyepatikana mara ya mwisho alishinda kipindi cha nusu bilioni kama hiki mnamo Aprili 2021.

Alikuwa ni Abdulaziz Ibrahim kutoka mkoani Tabora, Sikonge aliibuka mshindi wa Jackpot mara baada ya kubashiri kwa usahihi mechi zote 13 zilizowekwa kwenye Jackpot ya wiki hiyo.

Mpaka sasa SportPesa wameshatoa washindi zaidi ya saba wa Jackpot huku wakiendelea kutoa bonasi kila wiki kwa ajili ya washindi waliobashiri kwa usahihi kuanzia mechi 10 hadi 12.

Washindi wa SportPesa Jackpot kwa mara ya kwanza walipatikana mwaka 2019 Agosti ambapo Magabe Marwa na Kingsley Pascal waligawana 825,913,8640 Tsh baada ya Jackpot hii kukaa kwa miaka miwili.

Kwa mara ya pili na tatu walipatikana washindi wengine ambao ni Scolastika Ngwaluweson na Jamal Khalfan Abdallah ambapo waliondoka na kiasi cha shilingi 260,319,980 Tsh na 288,974,720Tsh kila mmoja.

Washindi waliofata ni Lilian Laizer na Yassini Ridhiwani ambao walijishindia 267,800,060 Tsh na 437,631,320 Tsh kila mmoja.

Unaweza kucheza na SportPesa kwa kubet Jackpot yao ili ujishindie Zaidi ya nusu bilioni kwa kutembelea webite yai ambayo ni www.sportpesa.co.tz au ponyeza hapa.

# El Classico kuchezwa Oktoba 24

**MADRID, Hispania**

WIKI ya kumi kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga, itashuhudia El Classico ya kwanza msimu huu kati ya Barcelona na Real Madrid ambayo itachezwa Oktoba 24, mwaka huu ikiwa ni siku ya Jumapili.

Real Madrid na Barcelona zina kampeni tofauti hivi sasa na Los Blancos ya Carlo Ancelotti imekaa juu ya jedwali la LaLiga, ikiwa alama mbili wazi, dhidi ya wapinzani wa jiji na mabingwa watetezi, Atletico Madrid.

Mchezo huo utapigwa kwenye dimba la Nou Camp, ambapo Real Madrid




atakuwa mgeni.

Wakati huo huo, Barcelona imeshinda mechi mbili tu kati ya nne za LaLiga msimu huu na kabla ya mechi yao na Cadiz, Blaugrana hao walikuwa alama nane nyuma ya Real Madrid na vita vilizuka kati ya kocha Ronald Koeman na Rais, Joan Laporta.

Timu zote mbili zinawasili kwenye El Clasico ya kwanza ya msimu, baada ya mechi za Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Real Madrid wakisafiri kwenda Shaktar Donetsk huko Ukraine Jumanne ya Oktoba 19, mwaka huu huku Barcelona kwa upande mwingine watawakaribisha Dynamo Kiev, Jumatano katika mechi ya kushinda baada ya kupoteza kwa Bayern Munich.

# 350,800 JACKPOT

## MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 25/09/21 | 17:00 | Leeds vs West Ham | 2.71 | 3.57 | 2.46 |
| 02. 25/09/21 | 17:00 | Watford vs Newcastle | 2.37 | 3.32 | 3.01 |
| 03. 25/09/21 | 17:00 | Blackpool vs Barnsley | 2.52 | 3.31 | 2.66 |
| 04. 25/09/21 | 17:00 | Swansea vs Huddersfield | 2.27 | 3.26 | 3.06 |
| 05. 25/09/21 | 17:00 | Nottingham vs Millwall | 2.81 | 3.05 | 2.56 |
| 06. 25/09/21 | 17:00 | Blackburn vs Cardiff | 2.34 | 3.24 | 2.95 |
| 07. 25/09/21 | 17:15 | Valencia vs Athletic Bilbao | 2.50 | 3.21 | 2.91 |
| 08. 25/09/21 | 18:00 | St Etienne vs Nice | 2.94 | 3.24 | 2.40 |
| 09. 26/09/21 | 15:00 | Mallorca vs Osasuna | 2.91 | 3.06 | 2.61 |
| 10. 26/09/21 | 16:00 | Southampton vs Wolverhampton | 2.57 | 3.22 | 2.82 |
| 11. 26/09/21 | 16:00 | Udinese vs Fiorentina | 2.66 | 3.31 | 2.66 |
| 12. 26/09/21 | 18:30 | Arsenal vs Tottenham | 2.41 | 3.17 | 3.07 |
| 13. 26/09/21 | 19:00 | Lazio vs Roma | 2.75 | 3.65 | 2.39 |

## MECHI ZA USHINDI


"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMAMOSI - 25 - SEPTEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 1748 | Chelsea vs Manchester City | 2.66 | 3.22 | 2.71 |
| 14:30 | 2587 | Reading vs Middlesbrough | 2.96 | 3.10 | 2.41 |
| 14:30 | 2786 | Manchester Utd vs Aston Villa | 1.45 | 4.67 | 6.72 |
| 15:00 | 4317 | Alaves vs Atletico Madrid | 6.42 | 3.91 | 1.55 |
| 16:00 | 2915 | Spezia vs AC Milan | 5.83 | 4.63 | 1.50 |
| 16:30 | 1642 | Eintracht Frankfurt vs FC Koln | 2.01 | 3.73 | 3.33 |
| 16:30 | 1964 | Hoffenheim vs VfL Wolfsburg | 2.74 | 3.44 | 2.44 |
| 16:30 | 2293 | RB Leipzig vs Hertha BSC | 1.33 | 5.21 | 8.21 |
| 16:30 | 2393 | Zenit St Petersburg vs Kryliya Sovetov | 1.34 | 5.15 | 7.53 |
| 16:30 | 4048 | Union Berlin vs Arminia Bielefeld | 1.68 | 3.73 | 4.97 |
| 16:30 | 5779 | Bayer Leverkusen vs Mainz | 1.75 | 3.94 | 4.19 |
| 17:00 | 1476 | Everton vs Norwich City | 1.63 | 3.88 | 5.44 |
| 17:00 | 1794 | Nottingham vs Millwall | 2.60 | 3.00 | 2.80 |
| 17:00 | 1973 | Birmingham vs Preston | 2.04 | 3.21 | 3.66 |
| 17:00 | 2555 | Dundee FC vs Rangers | 10.82 | 5.70 | 1.24 |
| 17:00 | 2861 | Motherwell vs Ross County | 1.72 | 3.65 | 4.53 |
| 17:00 | 2997 | Shakhtar Donetsk vs Veres Rivne | 1.17 | 6.19 | 12.58 |
| 17:00 | 3306 | Blackburn vs Cardiff | 2.24 | 3.26 | 3.11 |
| 17:00 | 3934 | Swansea vs Huddersfield | 2.41 | 3.11 | 2.96 |
| 17:00 | 4075 | Stoke City vs Hull City | 1.55 | 3.85 | 5.92 |
| 17:00 | 4402 | Leeds vs West Ham | 2.97 | 3.63 | 2.26 |
| 17:00 | 4422 | Watford vs Newcastle | 2.29 | 3.31 | 3.16 |
| 17:00 | 4702 | Bristol City vs Fulham | 4.54 | 3.50 | 1.76 |
| 17:00 | 5061 | Simba vs Young Africans | 1.50 | 3.20 | 3.30 |
| 17:00 | 5075 | Leicester vs Burnley | 1.59 | 4.02 | 5.63 |
| 17:00 | 5203 | Blackpool vs Barnsley | 2.45 | 3.15 | 2.86 |
| 17:00 | 5574 | Sheffield Utd vs Derby | 1.61 | 3.60 | 5.72 |
| 17:00 | 5685 | Hearts vs Livingston | 1.57 | 3.64 | 6.09 |
| 17:00 | 5707 | Bournemouth vs Luton Town | 1.60 | 3.91 | 5.14 |
| 17:15 | 5167 | Valencia vs Athletic Bilbao | 2.61 | 3.16 | 2.81 |
| 17:30 | 1747 | Willem II Tilburg vs PSV Eindhoven | 5.54 | 4.35 | 1.50 |
| 18:00 | 1287 | Slaven Belupo vs Dinamo Zagreb | 6.78 | 4.16 | 1.41 |
| 18:00 | 1939 | St Etienne vs Nice | 3.14 | 3.34 | 2.23 |
| 18:00 | 3380 | Wolfsberger AC vs RB Salzburg | 6.61 | 5.05 | 1.34 |
| 19:00 | 1007 | Inter vs Atalanta | 1.94 | 3.76 | 3.66 |
| 19:00 | 2403 | BSC Young Boys vs St. Gallen | 1.37 | 5.14 | 6.53 |
| 19:30 | 1958 | Brentford vs Liverpool | 6.23 | 4.42 | 1.50 |
| 19:30 | 3629 | Sevilla FC vs Espanyol | 1.61 | 3.82 | 5.83 |
| 19:30 | 3862 | Monchengladbach vs Borussia Dortmund | 3.87 | 4.27 | 1.75 |
| 19:45 | 2497 | Ajax vs Groningen | 1.03 | 12.79 | 34.44 |
| 19:45 | 4730 | Vitesse Arnhem vs Fortuna Sittard | 1.60 | 4.12 | 4.81 |
| 20:00 | 1435 | Vitoria Guimaraes vs Benfica | 4.92 | 3.79 | 1.64 |
| 20:00 | 5956 | Strasbourg vs Lille | 2.74 | 3.19 | 2.59 |
| 21:45 | 5110 | Standard Liege vs St Truiden | 1.96 | 3.49 | 3.59 |
| 21:45 | 5584 | Genoa vs Verona | 2.73 | 3.18 | 2.68 |
| 22:00 | 1502 | Feyenoord vs NEC Nijmegen | 1.19 | 6.68 | 11.80 |
| 22:00 | 3886 | Real Madrid vs Villarreal | 1.55 | 4.35 | 5.50 |
| 22:00 | 4676 | Utrecht vs PEC Zwolle | 1.28 | 5.52 | 8.87 |
| 22:00 | 5622 | Lyon vs Lorient | 1.38 | 4.99 | 7.19 |
| 22:00 | 5962 | Paris St Germain vs Montpellier | 1.26 | 6.13 | 9.02 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# MESSI KUIKOSA MANCHESTER CITY




**PARIS, Ufaransa**

MSHAMBULIAJI mpya wa PSG, Lionel Messi, anatazamiwa kuwa nje ya uwanja kwa takribani wiki mbili, baada ya vipimo vya MRI kuonyesha amepata mikwaruzo ndani ya goti lake la kushoto.

Messi aliumia kwenye mchezo wa Ligi Kuu Ufaransa, dhidi ya Lyon wikiendi iliyopita.

Kwenye mchezo huo, Kocha wa PSG, Mauricio Pochettino aliishuku afya ya nyota huyo na kuamua kumfanyia mabadiliko dakika ya 75 na nafasi yake ilichukuliwa na mlinzi wa kulia, Achraf Hakimi kwenye mchezo, ambao ulizua gumzo baada ya Messi kufanyiwa mabadiliko.

Messi tayari ameukosa mchezo mmoja wa Ligi Kuu Ufaransa, dhidi ya Metz uliokamilika kwa PSG kupata ushindi wa mabao 2-1 na kufikisha alama 21, kwenye michezo yake saba na kuwa na ushindi wa asilimia mia moja.

Maumivu ya goti yanayomkumba Messi yatakayomuweka nje kwa wiki mbili, yatamfanya akose mchezo mwingine wa ligi, dhidi ya Montepelier na hata ule wa Manchester City, kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya utakaochezwa Septemba 28, mwaka huu.

Wakati Messi anaumia, kiungo Maeco Verratti na mlinzi wa kati Sergio Ramos wameanza mazoezi ya kujiweka fiti zaidi, ili ajitupe dimbani.



# Koeman alia mwamuzi amemaliza Barca

**BARCELONA, Hispania**

KOCHA wa Barcelona, Ronald Koeman amesema waamuzi wa Hipsania wanaweza kukupa kadi nyekundu bila sababu, baada ya yeye na kiungo wake Frenkie de Jong kutolewa nje kwenye mechi iliyoisha kwa Barca kutoka suluhu na Cadiz, juzi Alhamisi.

Barcelona walihitaji kuondoka na ushindi katika dimba la Nuevo Mirandilla, lakini kadi nyekundu aliyopewa de Jong dakika ya 65, ilizima matumaini yao yote.

Miamba hiyo ya Katalunya hadi sasa wametoka sare katika michezo mitatu kati ya mitano ya LaLiga, wakiwa wamepitwa pointi saba na wapinzani wao Real Madrid wanaongoza msimamo.

Koeman kwa sasa mwelekeo wa kibarua chake, hauleweki katika viunga vya Katalunya baada ya kuanza msimu vibaya.

"Sitazungumzia matatizo yangu, inawezekana kubaki kama nitashinda na ikiwa nitaendelea kupoteza klabu haina budi kutafuta mkufunzi mwingine," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Nilisalimiana na Rais Joan Laporta muda mfupi kabla kuondoka hotelini, nina uhakika tutapata siku zaidi za kuzungumza, ikiwa klabu watataka kuzungumza."

Barcelona wanajiandaa na mchezo mwingine, dhidi ya Levante katika dimba la Camp Nuo, Jumapili hii.

# Michezo

Jumamosi Septemba 25, 2021

Nipashe



Messi kuikosa Manchester City UKURASA 23

AMEREJEA...




Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa Yanga, Senzo Mbatha (kulia), akimtambulisha rasmi Mkurugenzi mpya wa Maendeleo ya Soka la Vijana wa klabu hiyo, Mkongomani Mwinyi Zahera, ambaye aliwahi kuwa Kocha Mkuu kwenye timu yao. Yanga pia imemrejesha kundini Kocha, Cedric Kaze. **PICHA: MTANDAO**

## Africarriers yaipa Simba mabasi 3

**Na Saada Akida**

KATIKA kuendelea kujiimarisha kiuchumi, Kampuni ya magari ya Africarriers imeingia mkataba wa udhamini wa miaka minne na mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, wenye thamani ya Sh. milioni 800.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez, alisema jana jijini Dar es Salaam kupitia mkataba huo, klabu yao itapata vitu mbalimbali kutoka kwa wadhamini hao.

Barbara alitaja baadhi ya vitu ambavyo Simba itapata ni pamoja na basi aina ya Golden Dragon lenye uwezo wa kubeba watu 60, basi lingine aina ya Eicher lenye uwezo wa kubeba watu 45 na basi dogo aina ya Coaster.

"Basi kubwa litatumiwa na timu ya wakubwa, la watu 45 litatumiwa na Simba Queens na Coaster litatumiwa na timu ya vijana," alisema Barbara.

Mkuu wa Idara ya Sheria wa Africarriers, Ngassa Mboje, alisema pia kampuni hiyo itakuwa wadhamini wa mavazi wa timu ya vijana ya Simba.

"Ni jambo la fahari kwetu kuanza uhusiano huu na mabingwa wa kihistoria wa Tanzania. Tunaamini pande zote mbili zitanufaika na uhusiano huu," alisema Mboje.

Mkataba huo na Africarriers ni watatu kuingiwa na mabingwa hao mara nne mfululizo wa Ligi Kuu Tanzania katika kipindi cha mwezi mmoja.

Tayari Wekundu wa Msimbazi wameingia mikataba na Air Tanzania kwa ajili ya kuwasafirisha kwenye safari za ndani na nje ya nchi pamoja na Emirates itakayotoa tuzo kwa wachezaji watakaofanya vyema kila mwezi.

Wadhamini wakuu wa Simba ambao ndio klabu pekee Tanzania iliyobakia kwenye mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika ni SportPesa.

# WATANI WA JADI KUMALIZA UBISHI

## Makocha wafunguka huku vikao vya 'mauaji' vikiendelea kila...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

WASWAHILI wanasema usiku wa deni haukawii. Hatimaye siku ya mchezo wa kuwania Ngao ya Jamii kati ya Simba na Yanga uliokuwa unazungumziwa utachezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Mechi hiyo ni rasmi kwa ajili ya kufungua msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2021/22.

Inaweza ikawa mechi ngumu zaidi kuliko zilizopita, kwani timu zote zina wachezaji wapya kabisa waliosajiliwa kwa ajili ya msimu huu, na baadhi watakuwa wakicheza 'dabi' hiyo kwa mara ya kwanza.

Wachezaji wapya kwa Simba ambao huenda wakawa uwanjani leo ni pamoja na Pape Sakho, Sadio Kanoute, Peter Banda, Henoc Inonga, Duncan Nyoni, Kibu Denis na Israel Mwenda huku Fiston Mayele, Djuma Shaaban, Yannick Bangala, Jesus Moloko, Yusuph Athumani, Khalid Aucho na Djigui Diara kwa Yanga wakicheza dabi hiyo kwa mara ya kwanza.

Mara ya mwisho timu hizo zilikutana Julai 25, mwaka huu kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma ambapo Simba ilishinda bao 1-0, shukrani kwa beki Mganda, Thadeo Lwanga, lakini leo watani hao watakuwa wanakutana kwa mara ya tatu mwaka huu.

**Iwapo Yanga itashinda leo itaifikia Simba kwa idadi ya kutwaa ngao hiyo, kwani takwimu zinaonyesha wameshinda mara tano, huku Wekundu wa Msimbazi wakitwaa mara sita.**

Kuelekea mchezo wa leo, Kocha Mkuu wa Yanga, Nassredine Nabi amesema anafurahi kuwa miongoni mwa makocha watakaosimama katika mchezo huo ambao kwake ni mara ya tatu tangu alipotua hapa nchini.

Nabi alisema mechi hiyo ni muhimu sana kwake kwa sababu si tu 'dabi', bali ni fainali ambayo anatafuta bingwa atakayeanza msimu na taji mkononi.

"Siwezi kuahidi ushindi kwenye mchezo huo, nafanya kazi yangu ili kupata matokeo mazuri, tumeondolewa katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, inatulazimu kupambana kushinda mechi hii ili kuwapa furaha mashabiki na viongozi. Hakutakuwa na mabadiliko makubwa sana kwa sababu kuna changamoto kubwa ya kutumia wachezaji wa kigeni nane kati ya 12 tuliowasajili, " Nabi alisema.

Aliongeza wamejiandaa kupambana kuhakikisha wanapata ushindi ana imani na wachezaji wake licha ya bado hawajaungana na kutengeneza kombinesheni nzuri anayohitaji.

"Mashabiki watarajie kupata matokeo mazuri, nawapenda sana Wana-Yanga, wanipe muda na waniamini kwa sababu timu yangu inahitaji muda na kuwa bora zaidi ya ilivyo sasa," aliongeza kocha huyo.

Didier Gomes, Kocha Mkuu wa Simba alisema timu yake inauchukulia 'uzito' mkubwa mchezo wa leo kwa sababu wanahitaji ushindi na si pointi.

"Tutaingia na hesabu zetu, tutaingia tofauti na ambavyo wamewahi kutuona, ni mechi ninayohitaji matokeo, si mchezo wa kuangalia au kujaribu mtu," Gomes alisema.

Yanga itashuka uwanjani ikiwa na kumbukumbu ya kukosa taji lolote msimu uliopita wakati Simba ilitetea ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara na Kombe la FA.

Waamuzi wa mchezo huo wa watani wa jadi ni Ramadhani Kayoko atakayesaidiana na Frank Komba, Sudi Lila na Elly Sasii atakuwa mezani wakati Kamisaa ni Sarah Chao kutoka Manyara.

Katika kuhakikisha kila timu inapata ushindi, vikao vya viongozi na wanachama wa klabu hizo mbili vimeendelea kufanyika sehemu mbalimbali hapa nchini.

Baada ya mechi ya leo, Simba itaelekea Musoma kuwafuata wenyeji wao Biashara United wakati Yanga yenyewe itakwenda kwenye Uwanja wa Kaitaba kuwakabili Kagera Sugar.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >